

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 11 Juni, 2014**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza maswali na Ofisi ya Waziri Mkuu, atakayeuliza swali letu la kwanza Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa.

Na. 226

**Kumaliza tatizo la Uhaba wa Maji Chunya**

**MHE. VICTOR KILASILE MWAMBALASWA)** aliuliza:-

Upatikanaji wa maji kwa matumizi ya Binadamu na Mifugo Wilayani Chunya ni mdogo sana hasa katika Mji wa Chunya:-

Je, lini Serikali itamaliza kabisa tatizo la uhaba wa maji mjini Chunya.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa maji katika Mji wa Chunya ni asilimia 67.7 ikilinganishwa na lengo ambalo ni asilimia 95 kwa maeneo ya mjini. Hivyo, ni kweli bado iko changamoto ya upatikanaji wa huduma hii kwa wananchi. Ili kukabaliana na tatizo la maji katika mji wa Chunya, Serikali katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 ilitumia shilingi milioni 100 kwa ajili ya ukarabati wa mtandao wa maji kutoka kwenye kisima hadi kwenye tanki lililopo Mjini Chunya. Watu wapatao 14,074 wananufaika na mradi huu.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Aidha, kati ya mwaka 2011/2013, Serikali ilitumia shilingi milioni 68.0 kwa ajili ya uchumbaji wa visima eneo la Chokaa, ununuzi wa pampu 4 na viungio vyake. Utekelezaji wa mradi huu umeongeza uwezo wa mamlaka kuzalisha maji kutoka mita za ujazo 706 hadi 888.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Mamlaka ya Maji Chunya ilitengewa shilingi milioni 100 kutoka Wizara ya Maji kwa ajili ya uchimbaji wa visima vitatu na tayari visima hivyo vimechimbwa na vyote kwa ujumla vina uwezo wa kutoa maji mita za ujazo 23 kwa saa.

Katika kipindi hicho, Halmashauri ya Wilaya ya Chunya pia ilitenga shilingi milioni 60 kwa ajili ya ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji lenye mita za ujazo 90 katika mji wa Chunya. Ujenzi umefikia asilimia 80.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa muda mrefu, Serikali imekamaliza usanifu wa mradi mkubwa wa maji kutoka eneo la *Mining Safari* ambao umekadiriwa kugharimu shilingi bilioni 11.5 kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa huduma ya maji katika Mji wa Chunya. Mradi huu umeingizwa katika awamu ya pili ya utekelezaji wa *program Maendeleo* ya Sekta ya Maji inayotarajiwa kuanza Julai, 2014.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maji kwa ajili ya mifugo, Halmashauri kwa kushirikiana na TANAPA imechimba visima vitatu na kufunga pampu ya upepo katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya mifugo ambayo ni kijiji cha Shoga, Pembe na Kapalala. Visima hivyo vikikamilika vinakadiriwa kuhudumia mifugo zaidi ya 20,000.

Mheshimiwa Spika, hivyo endapo fedha zote zitapatikana na miradi yote iliyopangwa kukamilika, tatizo la maji katika mji wa Chunya litapungua kwa kiasi kikubwa. (*Makofi*)

**MHE. VICTOR KILASILE MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Ninakiri kabisa kwamba Serikali imekuwa ikitoa fedha kuweza kuchimba visima mjini Chunya, lakini mara nyingi visima hivi vinakuwa vinakauka baada ya muda mfupi sana. Kwa hiyo, bado wananchi wa Chunya wanashida sana ya maji na ikielewa kwamba Chunya ni kati ya miji ya kwanza ku-*develop* hapa nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi nina mpango wa kuenda kuchimba visima viwili mimi mwenyewe. Je, Serikali itanisaidia na kunichimbia kisima kingine kimoja? La kwanza hilo.

Pili, Serikali inasema ina mpango wa kutengeneza mradi kambambe kwenye Safari *Mining's* ambao utagharibu zaidi ya shilingi bilioni kumi. Wakati huo huo Serikali inatoa leseni za uchimbaji maeneo hayo hayo. Serikali inasemaje, kweli mradi huu utakuwepo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu kwamba Serikali inayo nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba tatizo la maji tunalitatua katika Wilaya ya Chunya na nimpongeze kwa jitihada zake anazozifanya za kuchimba visima viwili.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Sisi tutamsaidia pia kupata wataalam ambao watatafiti maji kuona kwamba visima hivyo havikauki, tutamsaidia hao wataalam na mambo mengine hayo tutaendelea kuongea naye kwa sababu tumetenga fedha bilioni 1.6 kwa Wilaya ya Chunya, kwa hiyo sisi tutaendelea kumupa ushirikiano. Pia ni kwamba, mpango ule kambambe utatelekezwa ambao utagharimu shilingi bilioni 11 ili kumaliza kabisa tatizo la maji katika mji wa Chunya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanjale, usiniambie wewe huko Chunya na wewe, haya.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, tatizo la maji katika miji mingi nchini limekuwa ni kubwa sana hasa miji hii midogo ambayo imeanzishwa sasa hivi, husasan Mji wa Mbalizi ambao pia umekuwa na matatizo ya maji kama Chunya.

Je, Serikali inasemaje kuboresha maji katika mji wa Mbalizi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale tumetoka kuongea sasa hivi na nimemwahidi kwamba tutakwenda katika Jimbo lake na matatizo mbalimbali ambayo ameongea.

Kwa hiyo, mimi ninamhakikishia kwamba tunayo nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba tunatatua tatizo la maji katika Mji wa Mbalizi. Pia, ziara iko palepale hasa alivyoongelea kuhusu ubora wa mabomba na kadhalika, tutamaliza tukiwa huko katika Wilaya yake. (Makofi)

Na. 227

### **Mamlaka ya Mji Mdogo Mombo**

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI (K.n. y. MHE. MARY PIUS CHATANDA)** aliuliza:-

Mji wa Mombo ulitangazwa kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo tangu tarehe 17 Septemba, 2004 lakini mpaka sasa haujapandishwa hadhi kuwa Halmashauri ya Mji licha ya taratibu zote za kupandishwa kuzingatia na kupelekwa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, ni lini sasa Mji huo utapandishwa hadhi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Spika, ni kweli mchakato wa kuanzisha Halmashauri ya Mji wa Mombo umepitika katika ngazi zote na maombi hayo yalishawasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) yakafanyiwa kazi kwa kuzingatia taratibu na vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria.

Taarifa zilizopo ni kwamba Timu ya Wataalam toka Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ilikwenda kufanya uhakiki mwezi Machi, 2014 kuangalia vigezo vya kupandisha hadhi Mamlaka hiyo kuwa Halmashauri ya Mji kama vimefikiwa na kama vinakidhi baada ya kupitishwa kwenye ngazi husika.

Mheshimiwa Spika, maombi haya yameshapokelewa katika Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na yamefanyiwa kazi kwa kuzingatia taratibu na vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria. Maamuzi na mapendekezo haya yatatolewa sambasamba na maombi ya maeneo mengine katika nchi yetu.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ninakushukuru sana kwa majibu yako mazuri na yenye matumaini sana kwa mji wa Mombo. Nina swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wewe na mimi yulienda wote na ukanifanyia kazi nzuri sana katika Jimbo langu hasa Mji wa Mombo. Na kwa kuwa Mheshimiwa Rais alienda pale akaongea na wananchi wa Mombo na akawapa matumaini baada ya ziara yake ya Mkoa wa Tanga atakuwa amemaliza jibu hili.

Na kwa kuwa mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi, wanaofanya uchaguzi pale ni Vitongoji, sasa ili wafanye Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Waziri ni lini Mji wa Mombo utaupandisha hadhi ili wananchi badala ya kufanya uchaguzi wa Vitongoji, wafanye uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumekwenda mpaka kule kwenye hii Mamlaka anayoizungumzia na sisi tunaotoka Mikoa ya Kaskazini tunapita pale kila wakati na wewe mwenyewe utakuwa unapafahamu. Ni mahali ambapo sasa ukiendelea kupafanya pakaendelea kuwa Mamlaka ya Mji wa Mdogo *is very unfair*.

Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge wote wawili Mheshimiwa Chatanda na Mheshimiwa Stephen Ngonyani kwa namna anavyolifuatilia hili jambo kwa karibu sana. Nakiri kwamba nimeona pia Ofisi ambayo wanajenga kwa ajili ya Mamlaka ya Mji Mdogo ile iliyopo pale ambayo huenda sasa wakaipanua kwa ajili kufanya Halmashauri ya Mji.

Nataka niseme hapa kwamba pia kuna maelekezo ya Mheshimiwa Rais ambayo ameyatoa hapa na kwetu sisi maelekezo ya Mheshimiwa rais ni Sheria. Kwa hiyo, tunakwenda kutekeleza kama alivyoelekeza hapa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu jana kwa Mheshimiwa Marombwe na wale wengine wote ambao wanakusudia kusimama hapa kwa ajili ya kuulizia Mamlaka hizi za Miji Midogo na Mamlaka na Halmashauri zenyewe.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Waziri Mkuu ameweka utaratibu mziru tunaangalia maeneo yote ya utawala sasa hivi tunavyozungumza, Vijiji, Kata, Wilaya pamoja na Halmashauri zote hizi zinazozungumzwa hapa.

Kwa hiyo, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Ngonyani kwamba hii kazi inakwenda vizuri na kama kungekuwa kuna mapungufu tungemuita tukamwambia kuna mapungufu lakini wale waliokwenda wataalam wame *indicate* kwamba, mji huu wa Mombo unastahili kuwa Mamlaka Kamili.

Mheshimiwa Spika, anachosema hapa ni kwamba waliopo pale wanaunda Mamlaka ya Mji Mdogo ni Wenyeviti wa Vitongoji yeye anataka anaondokane nao, anataka sasa awe na Halmashauri kamili kwa maana kwamba watakuwa na Bajeti yao wao wenyewe.

Mimi nataka kusema kwamba Mheshimiwa Ngonyani tutaendelea kushirikiana na wewe katika jambo hili hasa ukizingatia kwamba Mheshimiwa Rais alitoa tamko kuhusu Mji huu.

**SPIKA:** Yaani jibu si kwamba litapatikana, maneno mengi jamani. Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed.

Na. 228

### **Kujenga Viwanda vya Kusindika Nyama**

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED** aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kujenga viwanda vya kusindika nyama katika Mikoa yenye mifugo mingi ili kuinua kipato cha Wafugaji hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed (Viti Maalum) Kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ikishirikiana na Taasisi mbalimbali pamoja na sekta binafsi chini ya mpango wa *Private Public Partnership (PPP)*, imekuwa ikihamasisha ujenzi wa viwanda vya kusindika nyama katika maeneo yenye mifugo mingi ili kuwapatia wafugaji soko la mifugo na nyama safi na salama kwa soko la ndani na ziada kuuzwa nje ya nchi.

Jitihada hizi zimewezesha ujenzi wa viwanda ambavyo vimejengwa katika Jiji la Arusha (Sakina), Dodoma (*TMC Ltd.*), Sumbawanga (*SAAFI Ltd.*), Halmashauri ya Kilolo (*Mtanga Foods Ltd.*) na Magu (*Alpha Choice Ltd.*) ambavyo kwa pamoja vina uwezo wa kuchija, kuchakata na kusindika ng'ombe 1930 na mbuzi na kondoo 9,180 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, Viwanda vya *Tendaji Fods Ltd.* (Morogoro Vijijini) na *Triple S* (Manispaa ya Shinyanga) vinaendelea kukarabatiwa na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, Viwanda 5 vipya vya *Xinghua International Ltd.* (Shinyanga), Machinjo ya Ruvu (Bagamoyo), Machinjio ya Iringa (Manispaa ya Iringa) Kampuni ya Chobo (Jiji

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

la Mwanza) na *Manyara Ranch* (Monduli) vyenye uwezo wa kuchinja, kuchakata na kusindika ng'ombe 1,350 na Mbuzi na Kondoo 1,000 kwa siku vinaendelea kujengwa.

Aidha, kiwanda cha nyama cha Dodoma kinapanuliwa na kampuni za *Ali Kaffir Ltd.* (Oman) na *Furda Enterprises Ltd.* (China) kufikia uwezo wa kuchinja, kuchakata na kusindika ng'ombe 450 na mbuzi 2000 kwa siku. Viwanda hivi vitawezesha kuchinja, kuchakata na kusindika jumla ya ng'ombe 1,021,800 na mbuzi na kondoo 3,270,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizi, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara na kituo cha uwekezaji Tanzania yaani *Tanzania Investment Centre* inaendelea kuhimiza sekta binafsi kujenga viwanda katika Wilaya zenye mifugo mingi ili kuzalisha nyama safi na salama kwa walaji katika soko la ndani na ziada kuuzwa nje ya nchi. Nachukua fursa hii kuwahamasisha wafugaji kuzalisha mifugo bora na kuvuna kwa wakati ili kukidhi mahitaji ya viwanda hivi kuongezeka mwaka hadi mwaka.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rukia Ahmed!

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi, lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna kauli iliyozoeleka hapa kila siku mchakato bado unaendelea kutoka kwa Mawaziri wetu.

Je, Serikali inawambiaje wakulima na Wafugaji, viwanda hivi vitamalizika lini?

Pili, kwa kuwa nchi yetu ina tatizo kubwa la ajira. Je, Serikali imewaandaaaje vijana kuweza kuajiriwa katika viwanda hivi ili waweze na wao kujikwamua kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda nimuhakikishie kwamba hii lugha iliyozoeleka ya mchakato sasa inafikia mwisho, naomba mtuamini tumeanza kazi kwa nguvu mpya, kasi mpya katika Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Lakini katika suala zima hili la vijana kuajiriwa katika viwanda hivi, nitaliomba Bunge hili kwa sababu tunaendelea kuimarisha viwanda hivi ili kwa kweli kutoa ajira kwa Watanzania, tunataka kuhakikishia kwamba vijana watakaoleta maombi na kama watakuwa na sifa zinazotakiwa wataajiriwa katika viwanda hivi.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa viwanda ambavyo vimetajwa na Mheshimiwa Waziri kwamba vinakarabatiwa ni kiwanda cha *Triple S Shinyanga*. Habari ya kwamba kiwanda hiki

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

kinakarabatiwa imeanza kusikika siku nyingi sana zaidi ya miaka kama nane hivi iliyopita yaani 2007/2008. Nilitaka kujua hivi tatizo ni nini hasa ukarabati huu unachukua zaidi ya miaka 8?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maige kama ifuatavyo:-

Kiwanda hiki ni cha binafsi lakini kama mnavyofahamu kwamba sekta binafsi na kama nilivyoeeleza katika jibu la msingi siku hizi tunashirikisha kikamirifu Sekta binafsi katika mambo yote yanayofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa sababu tunatambua kwamba wanafanya kazi kubwa ya kutoa ajira katika kazi mbalimbali ambazo ziko chini ya sekta binafsi.

Kwa kuwa nitakwenda Kanda ya Ziwa hivi karibuni pamoja na Shinyanga na maeneo mengine, nitakwenda kufahamu tatizo hasa ni nini ili tuweze kuwasaidia ndugu zetu hawa waweze kutoa ajira katika viwanda vyao.

**MHE. MEDESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, itakubukwa Mbeya tulikuwa na kiwanda cha nyama, lakini hadi sasa hakifanyi kazi. Vilevile itakumbukwa kwamba Wilaya ya Mbarali ni miongoni mwa Wilaya zenye mifugo.

Je, wakati sasa umefika Serikali kuwashirikisha wafugaji ili kuona wanapata huduma hiyo ya viwanda vya mifugo ili waweze kuuza mazao yao kwa urahisi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, jibu ni ndiyo na tulishakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba nitatembelea maeneo yake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, hayo ndiyo majibu. Sasa tunakwenda Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana W. Kikwembe, atauliza swali hilo.

Na. 229

### **Kuhusu Mfumo Mpya wa Makusanyo ya Ushuru wa Forodha**

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE** aliuliza:-

Serikali kupitia TRA na Bandari imeanzisha mfumo mpya wa kutoa huduma ambao hauruhusu wakala na ofisa wa Ushuru kuonana, lengo kubwa likiwa ni kupunguza Rushwa.

Je, ni kwa kiasi gani rushwa imepungua tangu utaratibu huo uanze?

Je, kumekuwa na ufanisi kiasi gani wa makusanyo ya Ushuru wa Forodha toka utaratibu huo uanzishwe?

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa naibu Waziri majibu.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu A na B, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania imekuwa ikilalamikiwa sana kuhusu urasimu na ucheleweshwaji wa kuondoa mizigo bandarini, na pia mfumo wa malipo unaotoa mwanya mkubwa wa rushwa.

Ili kupunguza au kuondoa kabisa kasoro hizi, Mamlaka ya Mapato kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bandari Tanzania wameanzisha mfumo mpya wa usimamizi wa forodha ambao umekusudi akuondosha kero zilizokuwepo katika uondoshaji na ulipiaji wa mizigo iliyopo Bandarini.

Mfumo huo mpya ulikamilika mwezi Julai mwaka 2013 na kuzinduliwa rasmi mwanzoni mwa mwezi Ogasti mwaka 2013. Mfumo huo una uwezo wa kufanya mambo yafuatayo.

Kukusanya mahitaji ya watumiaji, kuchambua mizigo, ukaguzi, uondoshaji wa mizigo na abiria na usimamizi wa mnada na umma kwa mali zilizopitisha muda bila kuondolewa bandarini.

Mheshimiwa Spika, kipimo cha kiwango cha Rushwa katika vituo vyetu vya forodha ni kuangalia kama kuna uwezekano ama mianya ya walipa kodi na wafanyakazi waforodha kukutana kirahisi, na pia kama upo ucheleweshwaji na utoaji wa mizigo.

Tangu kuanza kwa maboresho ya mfumo wa makusanyo ya Ushuru wa Forodha ucheleweshaji wa mizigo umepungua kwa kiasi kikubwa, kwani hakuna sababu ya mtoza kodi na mlipa kodi, yaani wakala kukutana ana kwa ana; kutokana na ukweli kuwa nyaraka za mizigo zinawasilishwa kwa njia ya mtandao.

Mlipa kodi kujikadiria kodi mwenyewe, na endapo mteja amewasilisha taarifa sahihi kwenye mtandao sambamba na zile zilizowasilishwana Mamlaka ya Mapato Tanzania, malipo ya kodi hufanyika kwa njia benki na hivyo kuondoa kabisa fursa ya mtoza kodi na mlipa kodi na wakala wake kukutana ana kwa ana.

Mheshimiwa Spika, B, makusanyo halisi yanayotokana na ushuru wa forodha yameongezeka kutoka Shilingi bilioni tatu na milioni arobaini na mbili katika kipindi cha Julai-Aprili mwaka 2011/2012 hadi Shilingi bilioni nne na milioni mia moja arobaini na tisa katika kipindi hicho hicho kwa mwaka 2013/2014, ongezeko hili ni asilimia 36.4

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali napenda tu kufahamu mambo yafuatayo.



## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Katika mfumo huu imeonesha kwamba wakala na ofisa wa TRA hawakutani, na hivyo malipo yao na nyaraka nyingine kuwasilishwa kwa njia ya mtandao. Tumekuwa na tatizo kubwa sana la umeme na matatizo mengine yanayohusiana na mitandao kuwa chini.

Je, Serikali inasema nini kuondoa hii kero ili kuweza kumuondolea yule wakala aweze kufanya shughuli zake kwa haraka zaidi na kuweza kupunguza...

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili ningependa kumuuliza, kwa kuwa sasa hivi mfumo huu unahusisha pia na namna ya kuthaminisha mizigo, hasa inayoingia nchini ikiwemo pia bidhaa kama magari kutoka Japan.

Je, ni vigezo vipi vinavyotumiwa katika kuthaminisha bidhaa hizi, hasa ukizingatia kwa mfano kwa sasa hivi magari Japan yameshuka bei. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, yawe mafupi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Spika, hili la kuhusu upatikanaji wa umeme ama kukosekana kwa mtandao katika nyakati tofauti tofauti, Serikali imejipanga, kwanza katika vituo vya forodha vilivyo na u-busy kuongeza muda wa kufanya kazi, hivyo kama kuna wakati ambapo mtandao ulikuwa chini kazi hiyo iweze kufanyika wakati kuna mtandao. Kwa hiyo utaona kama Tunduma ama bandarini tumeongeza muda wa kufanya kazi kutoka ule wa kawaida mpaka masaa ishirini na nne.

Kuhusu hili la namna ya kukadiria, ni kweli kumekuwepo na malalamiko, lakini Mamlaka ya Mapato Tanzania inachokifanya ni kuhakikisha inapunguza udanganyifu.

Kwa hiyo kuna utaratibu ambao unaotumiwa wa *transaction data base*, kwamba kila biadhaa inayoagizwa inakuwa tayari iko kwenye mtandao, kwa hiyo Mamlaka ya Mapato na yenyewe inaweka bidhaa iliyoagizwa na kufanya ulinganifu na bidhaa hiyo hiyo ilivyoandikwa kwenye mtanda.

Kwa hiyo zile *case-by-case* zenyewe zinashughulikiwa zenyewe zinashughulikiwa kwa namna ya tofauti, ikitokea kwamba bidhaa iliyoagizwa haiku kwenye mtandao ama yenyewe imefanywa kuwa mtu na mtu kufanyiana biashara ya pamoja.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kumekuwa na hisia kwamba TRA imekuwa ikitumika kama fimbo ya adhabu kwa wafanyabiashara wanaokwenda kinyume na itikadi ya Chama cha Mapinduzi, nini ukweli wa suala hili.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Spika, si kweli, na si tu Mamlaka ya Mapato Tanzania bali Serikali yote inahudumia Watanzania bila kujali dini, rangi wala itikadi za kisiasa.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipatia nafasi. Kwa kuwa hakuna nchi yoyote inayoweza kuendelea bia kutoza kodi ya kutosha, na kwa kuwa tunatambua kuna mataifa mengi ambayo huhamasisha walipa kodi kwa kuwarudishia kiasi cha fedha ambacho wamelipia kodi kwa kuzingatia vigezo.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Sasa, Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haioni kwamba kuna haja sasa ya kufanya kama wanavyofanya wenzetu ili tuweze kuwahamasisha Watanzania kulipa kodi na hatimaye tuongeze pato la taifa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Leticia Nyerere kwa kutupa hiyo *experience* ya mataifa mbalimbali ya jinsi watu wanavyoona ni heshima kulipa kodi na ni wajibu na ni faida kwa taifa endapo kodi imelipwa; na Mamlaka ya Mapato Tanzania imeendelea kuboresha na kuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiari. Kila mmoja atambue kwamba ni wajibu wake, lakini vile vile ili taifa liendeleo linahitaji wananchi wake kulipa kodi.

Kwa hiyo kadiri tunavyoendelea na tunavyoboresha mifumo ya ulipaji kodi tutakwenda kwenye hizo hatua ambazo amependekeza Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo amenukuu kutoka maeneo mengine.

**SPIKA:** Ahsante, tuendeleo na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Susan Kiwanga atauliza swali linalohusika.

Na. 230

### **Kuhusu Wazee wa Mahakama ya Mwanzo Ifakara**

**MHE. SUZAN L. KIWANGA** aliuliza:-

Wazee wa Mahakama ya Mwanzo Ifakara hawajalipwa posho zao kwa muda mrefu sasa licha ya malipo hayo kuwa yameshaidhinishwa.

Je, ni lini Serikali itawalipa wazee hao haki zao?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA (K. n. y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suzan Limbweni Kiwanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea madai ya posho za Wazee wa Baraza wa Mahakama ya mwanzo Ifakara ya kiasi cha Shilingi milioni tatu laki mbili arobaini na saba na mia tano. Madai ya deni hilo yaliwasilishwa na kuorodheshwa katika orodha ya madeni ya mahakama kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, madai hayo hayakuwahi kuidhinishwa kwa ajili ya malipo kutokana na upungufu uliojitokeza katika nyaraka zilizowasilishwa na wazee wa mahakama ya mwanzo Ifakara. Upungufu huo ni pamoja na ukosefu wa viambatisho vya nyaraka muhimu vya kuwezesha malipo ya wazee wa baraza ambavyo vinaainisha jina la mzee wa baraza, aina na idadi ya kesi alizohudhuria, hukumu iliyotolewa na saini ya hakimu aliyesikiliza kesi hiyo.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mawasiliano yalifanyika ili mapungufu yaliyojitokeza yafanyiwe marekebisho na deni hilo liweze kulipwa. Aidha Wizara kupitia mahakama inafanya juhudi kuhakikisha kwamba madeni yote yaliyohakikiwa ya wazee wa mahakama yanalipwa, situ kwa mwahakama ya mwanzo Ifakara bali kwa mahakama zote nchini.

**MHE. SUZAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsantesana. Majibu ya Waziri yananisikitisha na ninatamani kulia. Mwaka 2011 thamani ya dola ilikuwa Shilingi 1,200, walikuwa wanadai milioni mia tatu na ushehe. Mwaka huu thamani ya dola inakuja 1,700, wamewakosea nini hawa wazee?

Sasa nataka kuihoji Serikali, mnataka muda gani ninyi mfanye huo upembuzi yakinifu kuhakiki haya madeni ili muwalipe hawa wazee ela zao?

Swali la kwanza, mnipe majibu ya usahihi. Sasa nataka kupata majibu ya uhakika, na wazee nchi nzima wanasikiliza, na si Ifakara tu nchi nzima, wamewakosea nini? Ndiyo maana rushwa mahakamani hazipungui...

**SPIKA:** Uliza swali si hotuba

**MHE. SUZAN L. KIWANGA:** ...inatisha sana, sasa anijibu tena, niulize swali la pili, kwamba ni lini sasa wazee nchi nzima na wa Ifakara watalipwa haya madeni yao wakati thamani ya Shilingi inazidi kushuka?

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa, wanalipwa kwa Dola kumbe, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA (K. n. y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Suzan Kiwanga kwa pamoja kama ifuatavyo;

Kama nilivyosema awali, tatizo wala halikuwa kwenye Serikali kuu huku. Makosa yalifanyika kule mwanzo na ndiyo maana yakarudishwa ili wafanye marekebisho, kwa maana ya yule Hakimu Mkazi wa Wilaya. Sasa Serikali ilikuwa inangojea marekebisho hayo ili sasa yahakikiwe ili waweze kulipwa.

Lakini nimtoe hofu tu kwamba kwa Mahakama hiyo ya Ifakara, pamoja na Mahakama zote za mwanzo za nchi nzima, tayari Shilingi bilioni moja nukta tano zimetengwa, ambazo zitalipwa kabla ya mwisho wa mwezi huu kwa madai yote yatakayokuja baada ya kuhakikiwa ili waweze kulipwa.

Kwa hiyo nina hakika kwamba kwa sababu imeshapelekwa ili wafanye huo uhakiki na kuleta nyaraka zinazohusika basi ndani ya bilioni moja nukta tano zilizotengwa kwa mwaka huu ambazo zitalipwa kabla ya mwisho wa mwezi huu, na hao mahakimu wa mwanzo wa Ifakara watalipwa na wengine wote nchini.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hawa wazee wamekuwa wakilipwa posho kiasi kidogo sana ukilinganisha na kazi kubwa wanayoifanya katika mahakama zetu za mwanzo, je ni lini sasa Serikali itawaongezea posho kubwa kiasi kutokana na kazi wanayoifanya?

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA (K. n. y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati kama ifuatavyo.

Ni kweli kwamba malipo ambayo wamekuwa wakilipwa hawa wazee wa baraza yamekuwa madogo, lakini Serikali imekuwa ikijitahidi kuongeza kadiri uwezo wa Bajeti unavyoruhusu.

Mtakumbuka tu kwamba ilikuwa ni 3,500, kwa sasa imeongezwa mpaka 5,000, na labda hiyo 5,000 bado ni kidogo. Serikali itaendelea kuangalia kadiri bajeti inavyoruhusu kadiri Bajeti inavyoruhusu kuona namna gani wanaweza kuongezewa tena.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa malipo ya posho za hao wazee wa mahakama huwa yana utata mara nyingi, napenda kujua, kwa niaba ya wazee nchi nzima, malipo haya ya Shilingi elfu tano yanalipwa kwa siku ama kwa kesi moja mpaka iishe?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA (K. n. y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana Chilolo kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hizi posho ni kwa siku lakini zitalipwa baada ya kesi kukamilika, si kwamba kwa siku basi analipwa hata kesi hiyo inaendelea. Kesi itakamilika lakini zitahesabiwa siku ambazo amehudhuria katika kesi hiyo ambayo sasa itakuwa imekamilika. Kwa hiyo ni kwa siku lakini mpaka kesi zikamilike.

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu hapa kwamba kuanzia mwaka ujao wa fedha hawa wazee sasa watakuwa wanalipwa moja kwa moja kwenye akaunti zao, na Wizara saa hivi imeshaitisha wapate nyaraka zote za hawa wazee, ikiwemo akaunti zao za benki ili baada ya uhakiki wa fedha zao zilipwe moja kwa moja kwenye akaunti zao badala ya kupeleka kwenye Sekretarieti ya Mahakama ya Mkoa ili wao wazipeleke kule kwenye mahakama za mwanzo. Watakuwa wanalipwa moja kwa moja kwenye akaunti zao.

**SPIKA:** Ahsante sana, waheshimiwa tuko ndani ya Bunge, maana watu hata haya maswali yanayoulizwa hapa hawasilizi kabisa. Kwa hiyo ninaendelea, Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Ezekiel Maige atauliza swali linalofuata.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kuuliza swali langu nilikuwa naomba nifanye marekebisho kidogo, kwenye mstari wa mwisho kabla ya zile A, B na C.

Na. 231

### **Kuhusu Mikataba ya Madini Kukosesha Halmashauri Mapato**

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE** aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Kahama imeshindwa kukusanya ushuru wa huduma toka migodini unaofikia Dola 7,406,992.7 kutokana na Serikali kufunga mikataba ya uendeshaji wa migodi ya Bulyanhulu na Buzwagi na kuvunja Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa inavyoruhusu

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Halmashauri kutoza ushuru wa huduma usiozidi asilimia sifuri nukta tatu ya thamani ya mauzo (0.3%).

Je, Serikali inaisaidiaje Halmashauri ya Wilaya ya Kahama ili ilipwe haki yake?

Je, Serikali itarekebisha lini kasoro hiyo kwenye mikataba iliyovunja sheria?

Je, Serikali itatekeleza lini ahadi yake ya kuleta mikataba Bungeni ili Wabunge waone kama ina maslahi kwa Taifa?

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES MUHANGWA KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige lenye sehemu a, b na c, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, sehemu (a) ni kweli kwa mujibu wa mikataba ya uendeshaji wa migodi, kumeonekana kuwa na upotevu wa mapato ukilinganisha na mapato ambayo yangepatikana kupitia ushuru wa huduma kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982.

Wizara yangu inaendelea kulifanyia kazi tatizo hili na kwa sasa baadhi ya wawekezaji wameanza kulipa malimbikizo ya ushuru wa huduma.

Kwa mfano mwaka 2013 wawekezaji wa *African Barrick Gold* walilipa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama jumla ya Dola za Marekani laki tisa thelathini na nne.

Majadiliano yanaendelea kufanyika kati ya Serikali na ADG ili kuona jinsi ya kumaliza deni hilo na kubadili kipengele husika cha mkataba ili waanze kulipa ushuru wa huduma kwa mujibu wa Sheria za Serikali za mitaa ya mwaka 1982, yaani asilimia 0.3 ya thamani ya mauzo ya madini. Majadiliano na wawekezaji wengine pia yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu (b), napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa urekebishaji wa mikataba iliyopo unaendelea kufanyika kwa awamu tangu Bunge lilipotunga Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. Ilianza kutumika tarehe 6 Oktoba, 2010. Serikali ilianzisha majadiliano na kampuni zote zenye mikataba ya uendeshaji wa migodi, ambapo migodi yote inaendelea kukubaliana na matakwa ya sheria hiyo, ikiwemo kulipa mrabaha wa asilimia nne ya mapato badala ya kiwango cha zamani cha asilimia tatu ya *net-back value*.

Ni matarajio yetu kuwa wamiliki hao wa migodi watakubali pia kuanza kulipa ushuru wa huduma kwa asilimia 0.3 ya mapato kama sheria husika inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, Sehemu (c). kuhusu ombi la mikataba kuletwa Bungeni Serikali imekuwa ikitoa ufafanuzi kuwa Mkataba ni baina ya pande mbili, yaani Serikali na mwekezaji, hivyo kuna utaratibu wa kufuata ili kuipata mikataba hiyo.

Aidha, tumekuwa tukitoka ufafanuzi kuwa mikata hii si siri kwa Waheshimiwa Wabunge kwani inapatikana Wizarani, na pia Kamati zote za Bunge zilizowahi kushughulikia masuala ya madini zilipewa nakala ya mikataba hiyo kwa ajili ya rejea na kumbukumbu.

Pia nakala ya mikataba yote ya uendelezaji wa migodi zimehifadhiwa kwenye maktaba ya Ofisi ya Bunge.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**SPIKA:** Hajjahifadhiwa, kinachotokea ni kwamba yule anayetaka mkataba anaandika Ofisi ya Bunge, Ofisi ya Bunge ndiyo inakwenda kuuchukua mkataba huo na kumpa yule aliyetaka huo mkataba, ndiyo utaratibu. Mheshimiwa Ezekiel Maige.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Lakini kipekee nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri Stephen Masele, kwa jinsi alivyosimamia majadiliano kwenye eneo hili ambalo ninakiri kwamba kwenye hotuba ya Serikali wamekubali kwamba Mwekezaji ataanza kulipa hii asilimia 0.3 kuanzia mwaka huu.

Pamoja na shukrani na pongezi hizo naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa upungufu wa malipo haya, yaani 0.3, kwa mfano kwa mgodi wa Bulyanhulu imekuwa hailipwi toka mwaka 2001 mgodi ulipoanza uzalishaji, na mwekezaji amekubali kuanza kulipa mwaka huu 2014. Kwa hiyo kuna miaka 13 ambayo hajalipa. Nilitaka kujua kama Serikali iko tayari kuendelea kufanya naye majadiliano ili aweze kulipa kwa sababu jumla ya fedha ni zaidi ya dola milioni nane, ambazo ni deni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Katika makubaliano ya kimkataba na ya kisheria yaliyoko kati ya Mgodi na Serikali ni pamoja na Mgodi kutoa huduma za kijamii, yaani *social responsibility*; na mgodi wa Bulyanhulu wakati wanaanza kampeni zao ili wakubalike kwenye jamii mwaka 1996 waliahidi mambo mengi ikiwa ni pamoja na kujenga barabara ya lami kati ya Kahama na mgodini, kujenga chuo cha ufundi (VETA), hospitali yenye hadhi ya wilaya pamoja na maji ya Ziwa Victoria, yote hayo hayajatekelezwa.

Nilitaka kujua Serikali inafanya nini ili kusimamia makubaliano haya baina ya wananchi na mgodi yatekelezwe?

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi, Serikali inaendelea kujadiliana na ABG, kuhakikisha kwamba, malimbikizo ambayo hayakulipwa kulingana na Sheria ya Ushuru huu wa 0.3, yanaendelea na kama nilivyosema, tayari wameshaanza kulipa. Kwa hiyo, mazungumzo yanaendelea.

Kuhusu, mgodi kutoa huduma za jamii, nimhakikishie Mheshimiwa Maige kwamba, tunaendelea kuzungumza na ABG, kuendelea kuhakikisha kwamba, ahadi zote ambazo wamezitoa, ziweze kutekelezwa kama ambavyo sasa hivi katika Mgodi wa kule North Mara, asilimia kubwa ya ahadi zao wamezitekeleza.

Na. 232

### **Umiliki na Utoaji wa Leseni za Madini ya "Moram"**

**MHE. GRACE S. KIWELU (K.n.y. MHE. FREEMAN A. MBOWE)** aliuliza:-

Mlima Boro ulipo Jimbo la Hai, Kata ya Masama Kusini, Kijiji cha Kware ni chanzo cha madini ya "Moram" yanayotumika katika ujenzi wa barabara mbalimbali:-

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

(a) Je, ni nini Sera ya Serikali kuhusu umiliki na utoaji wa leseni wa madini ya aina hii na ni nani ambaye amepewa leseni ya uchimbaji na kufaidika na mapato ya rasilimali hii?

(b) Je, Kijiji cha Kwale na Kata ya Masama Kusini wamenufaikaje kwa miaka kumi iliyopita kutokana na uvunaji wa rasilimali hii katika eneo lao?

(c) Je, Halmashauri ya Wilaya ya Hai ambapo ndipo Hazina hii ilipo ina haki gani katika kutumia rasilimali hii?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Freeman A. Mbowe, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Kwale kilichoko katika Kata ya Masama Kusini, Jimbo la Hai, kina historia ya muda mrefu ya uchimbaji wa madini ya ujenzi. Uchimbaji huo kwa miaka mingi ulikuwa unafanywa na Idara ya Ujenzi kwa ajili ya shughuli za ujenzi wa barabara. Kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010, mtu yeyote ambaye hana kizuizi cha kisheria, anaweza kuomba na kumilikishwa leseni ya uchimbaji wa madini ya ujenzi, mahala ambapo hapana leseni nyingine. Kwa sasa katika eneo la Kijiji cha Kwale kuna leseni tatu za uchimbaji madini ya ujenzi, zinazomilikiwa kwanza na TANROAD, pili na Bwana James Munuo na mwenzake Isack Ndashauka. Wamiliki wa leseni hizi wanalipa ada za leseni na mirabaha, kutokana na uzalishaji kwenye Ofisi yetu ya Madini Arusha.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali za Mitaa, kama Vijiji, Kata na Halmashauri za Wilaya, zinaweza kunufaika na uvunaji wa madini ya *moram* kwa kutoza ushuru wa huduma kwa kampuni au wamiliki wa leseni katika maeneo husika. Aidha, vijiji hunufaika na fursa za ajira na biashara zinazoweza kupatikana katika maeneo ya uchimbaji. Wizara itafuatilia kuona hali halisi ya manufaa katika Kijiji cha Kwale, ambapo kuna leseni tatu za uchimbaji madini.

(c) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Hai, inaweza kutumia rasilimali hii kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Madini. Kama ilivyo kwa TANROAD, Idara husika ya Halmashauri ya Wilaya, inaweza kuomba kumilikishwa leseni katika eneo hilo la wazi.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(i) Je, ni lini sasa; ningelipenda kujua *commitment* ya Serikali itafuatilia na kuleta majibu hapa ili kujua Kijiji hiki cha Kwale kimekuwa kikinufaika na nini; kwa sababu Wizara imekuwa ikikusanya ushuru kupitia Ofisi ya Madini, Mkoa wa Arusha; ni lini tutapata kujua majibu hayo?

(ii) Halmashauri yetu ya Hai, mapato yake ya ndani ni kidogo sana. Je, Serikali itakuwa tayari kufuta leseni hizo tatu na kuipa Halmashauri Mradi huo tuweze kuongeza mapato yetu ya ndani katika Halmashauri yetu ya Hai?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kabla hujajibu swali hilo; Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 66.(3)(b), ninaomba mnisikilize inasema hivi: "Mbunge aliyepo Bungeni wakati wa mjadala, atakuwa anatulia na kukaa kwa heshima mahali pake na hatatangatanga kwenye Ukumbi wa Mikutano bila sababu."

Kuna watu wanatangatanga bila sababu katika Ukumbi wa Mikutano, sasa nitakuwa ninawataja. *(Kicheko/Makofi)*

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu maswali hayo!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Grace Kiwelu, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyojibu katika swali la msingi; cha kwanza kabisa ni wajibu wa Halmashauri kuhakikisha kwamba, inatumia fursa zilizopo katika maeneo husika. Kwa hiyo, cha kwanza ambacho wanapaswa kufaidika nacho ni ile 0.3 ambayo wanapaswa watoze. Wanapaswa watoze hii baada ya kuwa na sheria ndogo ndogo ambazo watakuwa wamezitungeneza katika Halmashauri yao. Kwa hiyo, niwaombe kwanza, watengeneze hizo sheria ndogo ndogo ili ziwawezeshe kuweza kufaidika na hii 0.3. Sisi tutaendelea kushirikiana nao kwa pamoja ili tuone ni kwa namna gani tunaweza tukaharakisha jambo hilo.

La pili, kuhusu kufuta hizi leseni, niseme tu kwamba, kuna utaratibu na kuna sheria ambazo zinamlinda mwenye leseni. Kwa hiyo, haitakuwa jambo jema kwa Serikali kuwafutia hawa, halafu kuwapa Halmashauri. Nishauri tu Halmashauri ya Hai, iangalie sehemu ambazo hazina leseni, basi iombe leseni hizo ili iweze kupatiwa.

**SPIKA:** Ninaomba tuendelee na swali la Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, atauliza swali hilo!

Na. 233

### **Tatizo la Ujenzi Holela Mijini/Vijijini**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA** aliuliza:-

Ili kuondoa tatizo la ujenzi holela mijini na vijijini, kwa nini Serikali isiwe na mpango wa kupima ardhi na kuweka miundombinu ya maji, barabara na mitaa pamoja na usimikaji wa nguzo za umeme kama nchi nyingine wanavyofanya?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa tatizo la ardhi isiyopimwa, ambapo hadi sasa takribani asilimia kumi tu ya ardhi ndiyo iliyopimwa nchini. Pia Serikali inatambua kuwa, nchi yetu inakabiliwa na tatizo sugu la ujenzi wa makazi holela mijini na vijijini, ambao unatokana na upungufu wa viwanja vilivyopimwa na miji, ama kutokuwa na mipango kabambe ya uendelezaji (*Master Plans*) au mipango hiyo kutofuatwa kabisa. Sheria ya Mipango Miji Namba 8 ya Mwaka 2007, inatamka wazi kuwa, ujenzi wa nyumba mijini ni sharti upate kibali cha ujenzi (*Building Permit*), kabla ya ujenzi kuanza. Jambo hili lingezingatiwa, tusingekuwa katika hali mbaya tuliyonayo kutokana na ujenzi holela.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa tatizo hili, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imeanza utekelezaji wa kupima kila kipande cha ardhi nchini, ambapo mpango huu umeanza katika Wilaya ya Mvomero. Matarajio ni kwamba, ifikapo mwaka 2017, kila kipande cha ardhi, kitakuwa kimepimwa nchini, kupitia Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now*).



## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana kabisa na wazo zuri la Mbunge kuhusu Serikali, yaani Halmashauri na Taasisi nyingine za TANESCO, Barabara na Maji, kushirikiana kwa pamoja kuweka miundombinu wakati wa utekelezaji wa Miradi ya Upangaji Miji na Upimaji. Changamoto inayoikabili Serikali ni ufinyu wa Bajeti pamoja na kuhakikisha kuwa, Wananchi wetu wenye kipato cha chini, wanapewa viwanja kwa gharama nafuu. Hata hivyo, Serikali italitazama kwa upana wake na kisha kuchukua hatua stahiki.

Kwa kuwa Halmashauri zilizoanza zoezi la upimaji wa viwanja vyenye miundombinu (*Sites and Services*), zinatamia pesa za mikopo ya Benki za Biashara. Viwanja hivi sasa vinakuwa aghali. Serikali inaangalia uwezekano wa kutatua tatizo hili kwa kuboresha Mfuko wa Kuzikopesha Halmashauri moja kwa moja. Ni muhimu kwa Halmashauri zilizokopesha na bado hazijarejesha mikopo kufanya hivyo. Aidha, Halmashauri zitambue umuhimu wa kutenga Bajeti ya Mipango Miji kuliko kusubiri ruzuku ya Serikali Kuu.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali ya nyongeza. Kabla sijauliza, ninashukuru Serikali imekiri kwamba, Sheria ya Mipango Mijii haifuatwi, wala Mipango Kabambe ya Uendelezaji wa Mijini hakuna.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Baraza la Taifa la Takwimu, Watanzania sasa tunaongezeka kwa asilimia 2.7. Maana yake ni kwamba, tunaongezeka lakini ardhi iko vilevile.

(i) Je, Serikali haioni kwamba kwa kutopima ardhi ili itambulike matumizi yake kunaendelea kusababisha migogoro kati ya Wawekezaji na Wananchi; Serikali kwa maana ya maeneo ya Hifadhi na Wananchi; na vilevile Wakulima na Wafugaji na Wananchi wataendelea kufa?

(ii) Serikali imekiri kwamba, ufinyu wa Bajeti ndiyo unaosababisha ardhi kutokupimwa na imepimwa kwa asilimia kumi tu. Tumeshuhudia maeneo mengi sasa hivi Serikali ilishapima ardhi, lakini bado inaenda kuyachukua tena na kutaka kuwalipa Wananchi fidia; hali inayoleta mzozo nchi nzima. Sasa mmesema kufikia 2017, mtakuwa mmepima ardhi yote. Mtatumia mikakati gani kuhakikisha mnakamilisha zoezi hilo wakati inaonekana kabisa Bajeti siyo halisia? Ukiangalia Bajeti ya Serikali kwa upande wa Maendeleo kwa Wizara yako kazi zote ni shilingi 34,379,977,000 mtatekelezaje? Tunaomba kujua mipango yenu. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, hali ya sasa hivi ya kutokuwa tumepima ardhi, kama nilivyosema, asilimia kumi ndiyo iliyopimwa, kwa sababu hiyo ndiyo hali halisi ya Bajeti tuliyonayo. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hali itakaporuhusu, bajeti ikapatikana, ardhi itapimwa na chini ya *Big Results Now*, ambao ni mkakati wa Serikali kuhakikisha mambo muhimu yanakwenda mbele, nina imani kabisa kazi hii itatekelezwa.

Kuhusu swali lake la pili, Serikali kupima halafu ikatwaa ardhi; nifafanue tu kwamba, wakati mwingine kwa manufaa ya umma, Serikali hulazimika kutwaa ardhi chini ya Sheria Namba 47 ya Mwaka 1967 ya Utwaaji wa Ardhi. Sheria ya Ardhi inamlinda mwenye ardhi hiyo inayotwaliwa, iwe imepimwa au haijapimwa kwa kutoa fidia stahiki.

Mheshimiwa Spika, hilo ndiyo jibu.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Ninaomba nimwulize Mheshimiwa Waziri, swali dogo la nyongeza.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Kwa kuwa Halmashauri nyingi zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa vifaa vya kupimia ardhi na hivyo kuchukua Wataalam wa Makampuni Binafsi na baada ya upimaji gharama inakuwa kubwa sana kwa Wananchi kununua viwanja hivyo. Ninataka nifahamu Serikali ina mpango gani wa kupeleka vifaa vya upimaji ardhi kwenye maeneo ya Wilaya ili kazi hiyo ifanyike kwa urahisi na gharama ya viwanja iwe nafuu kwa Wananchi?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa sasa teknolojia ya upimaji wa ardhi imekwenda mbele sana. Sasa hivi tunao uwezo wa kupima ardhi kwa kutumia kipimo cha GPS au kupima moja kwa moja kwa kutumia picha za anga. Niseme tu kwamba, vifaa vyenyewe sasa hivi Serikali iko mbioni kutoa mafunzo kwa Maafisa Ardhi na Wapima, kuweza kuingia katika teknolojia ya kisasa. Hata hivyo, nitoe angalizo kwamba, upimaji wa ardhi unaandamana na upangaji wa ardhi. Kwa hiyo, unakuta lazima upange kwanza halafu ndiyo upime na ukishapima unamilikisha. Kwa hiyo, siyo tukio ni mchakato ambao unachukua muda, lakini Serikali inatambua uwepo wa teknolojia na itasaidia sana kasi ya kupima ardhi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

Mheshimiwa Spika, swali la msingi linasema kupima ardhi na kuweka miundombinu ya maji, barabara na kadhalika. Sasa pamoja na tatizo la kutokupima, lakini kuna tatizo la maeneo yaliyopimwa kutokupelekewa huduma hizi muhimu; mfano ni Kata ya Isyesye - Makazi mapya Mbeya Mjini, pamoja na Kata ya Itezi. Watu wamejenga nyumba nzuri lakini hakuna umeme, maji wala barabara wakati wa masika. Bila umeme usalama unakuwa tatizo kila siku watu wanavamiwa.

Ninafikiri Halmashauri ya Jiji imeshindwa; Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha maeneo kama haya ya Isyesye mpya pamoja na Itezi yanapelekewa huduma stahiki kwa usalama wa raia?

**SPIKA:** Swali lako zuri, lakini maeneo uliyoyataja Waziri hatayajibu. Jibu tu *principle* inayohusika. Ninakuomba ujibu hivyo basi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba niseme kwamba, katika sehemu nyingi hizo *sites and services* bado hazijakamilika. Nielezee kwamba, jukumu hili Halmashauri zetu zinahimizwa pale zinapopima viwanja ziweke pia Miundombinu. Katika jibu langu la msingi nimeelezea kwamba, kazi ya upimaji wa ardhi pia inaendana na Taasisi na Idara nyingine husan TANESCO, Idara ya Maji, kusudi ikae vizuri.

Sasa maeneo ya Mbeya, ninakubali inawezekana hawajapata hiyo miundombinu, lakini siyo Mbeya peke yake, ni sehemu nyingi. Halmashauri zetu zinatakiwa kufanya inavyotakiwa hasa wanapotumia kampuni za kupima, maana tozo inakuwa kwa ajili ya miundombinu pia.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninawaomba tuendelee na Wizara ya Uchukuzi. Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, atauliza swali hilo!

Na. 234

**Marubani Wanaorusha Ndege**

**MHE. AMINA ADBALLAH AMOUR** aliuliza:-

Ndege zinazoruka ndani ya nchi huendeshwa na Rubani mmoja:-

(a) Je, inapotokea Rubani ameshindwa kuendesha ndege hiyo kwa sababu za kiafya huku akiwa angani inakuwaje?

(b) Je, kwa nini Serikali inaruhusu Rubani mmoja kurusha ndege pasipo msaidizi?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, swali lake lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba, ndege zote zinazoruka ndani ya nchi huendeshwa na rubaini mmoja. Ndege zote kubwa za abiria zinazotoa huduma ya usafiri wa ratiba (*Schedule Flights*) ndani ya nchi, kwa mfano, *ATRA 42, ATR 72, CRJ 200ER, Airbus 319-200, Bmbadier Q-300 Dash 8*, ni lazima kwa mujibu wa Kanuni za Usafiri wa Anga zirushwe na marubani wawili wawili. Aidha, lipo kundi la ndege ndogo zinazobeba abiria nchini ambalo limegawanyika sehemu mbili kama ifuatavyo:-

(i) Ndege ndogo zenye uzito wa kuondokea wa kila 5,700 (*Maximum Certified Takeoff Mass*) au zaidi, lazima kisheria zirushwe na marubani wawili.

(ii) Ndege zenye uzito wa kuondokea chini ya kilo 5,700 na zisizochukua zaidi ya abiria tisa, zinaweza kururushwa na Rubani mmoja lakini kwa sharti kwamba, Rubani huyo awe amevaa *headset* na ndege yake ina *digital map display*. Hata hivyo, Rubani mzoefu anaweza kuruka bila vifaa hivyo, lakini kwa Kibali Maalum cha Mamlaka ya Usafiri wa Anga (*TCAA*).

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza, ndege ambazo huweza kurushwa na Rubani mmoja ni ndege ndogo na haziruki juu sana wala kusafiri masafa marefu. Endapo Rubani atapata tatizo la kiafya wakati akiwa angani, amefundishwa mbinu za kufanya zikiwemo kutafuta kiwanja kilicho karibu au eneo lililo salama na kutua. Aidha, ndege zinazoendeshwa na Rubani mmoja huwa zimetengenezwa mahususi tangu kiwandani ili ziendeshe na rubani mmoja mmoja na uendeshaji wake kama nilivyoeleza, unasimamiwa na sheria.

**MHE, AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Katika majibu yake ya msingi, ninaomba niyasome kwa ruhusa yako; ndege ambazo huweza kurushwa na Rubani mmoja ni...

**SPIKA:** Hapana uliza swali huwezi kusoma tena majibu.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Ndege ambazo zinarushwa na rubani mmoja ni ndogo na marubani wameelekezwa vitu vya kufanya ikitokea dharura. Swali langu:-

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

(i) Pindi Rubani huyu akifa akiwa angani maelekezo hayo hii ndege itaweza kushuka bila Rubani? *(Kicheko)*

(ii) Kwa nini au kuna uzito gani hata hizi ndege ndogo zikawekwa Marubani wawili?  
**SPIKA:** Hiyo ni hofu ya kifo tu, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Amina Amour, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la afya za marubani walio kazini linachukuliwa umuhimu wa juu sana na mamlaka ya udhibiti wa usafiri wa anga. Marubani hawa hupimwa afya zao mara kwa mara, wanathibitishwa kabla hawajaruka na hutoa taarifa zao kwa mamlaka katika muda ambao umetajwa kisheria.

Suala lingine nililolisema katika jibu langu la msingi ni kwamba, endapo wamefundishwa, akijisikia vibaya atatoa taarifa na atawasiliana na waongozaji wa ndege ili aelekezwe mahali mahali pa karibu pa kutua.

Mheshimiwa Spika, siyo ndege ...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mmeanzisha mchezo usiokuwa sawasawa; endelea kujibu!

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Siyo ndege zote zilizotengenezwa hapa Duniani zina viti viwili. Nimesema hapa, zipo ndege zinazotengenezwa mahususi kurushwa na Rubani mmoja. Hao waliotengeneza walijua sana kwamba, hayo majanga ya mtu kupatwa na ugonjwa na kadhalika, yanaweza kutokea, lakini hatua za kiusalama na ndiyo maana mpaka leo hatujawahi kuwa na tukio la Rubani kufariki akiwa angani.

**SPIKA:** Ahsante. Msije mkatutisha kupanda ndege bure, afadhali tuendele. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Abbas Zubeir Mtemvu, swali linalofuata; Mheshimiwa Mtutura kwa niaba yake.

Na. 235

### **Kampuni ya Ndege ya Fastjet**

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA (K.n.y. MHE. ABBAS ZUBEIR MTEMVU)** aliuliza:-

Imefahamika kuwa Kampuni ya Ndege ya *Fastjet* imesajiliwa hapa nchini:-

Kama hivyo ndivyo; je, kwa nini kampuni hiyo isifanye safari za nje ya nchi kama vile Afrika Kusini, Falme za Kiarabu, Qatar, Uingereza na nchi nyinginezo?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Abbas Zubeir Mtemvu, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Ndege ya Fastjet mbali na kusafirisha abiria kati ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere cha Dar es Salaam na Viwanja vya Ndege vya KIA, Mwanza na Songwe, inafanya vilevile safari za kutokea Julius Nyerere International Airport kwenda Johannesburg mara tatu kwa wiki na inatokea Julius Nyerere mpaka Lusaka mara tatu kwa wiki vilevile.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa, Kampuni ya Fastjet haijafikiria kuanzisha safari za kwenda katika Nchi za Falme za Kiarabu, Qatar au Uingereza kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge. Pindi Kampuni itakapoomba kufanya hivyo, Wizara ya Uchukuzi itatoa ushirikiano unaostahili kwa Kampuni hii ili iweze kutimiza azma yake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtutura swali la nyongeza!

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

(i) Mheshimiwa Spika, kazi kubwa ya Serikali ni kuandaa mazingira rafiki ili makampuni yaweze kufanya biashara, hasa ukizingatia kwamba, Watanzania wengi sasa hivi wanafanya biashara kubwa kati ya Tanzania na nchi za Kiasia, ilikuwa ni jukumu la Serikali kuweka mazingira rafiki ili Kampuni hii iweze kuvutika kupeleka ndege zile kule kwa sababu zinatoa bei nafuu sana kuliko makampuni mengine. Je, Serikali iko tayari kuandaa mazingira hayo? *(Makofi)*

(ii) Kampuni ya Fastjet imekuwa ikitoa huduma katika Miji ya Mbeya, Arusha pamoja na Mwanza. Je, sasa hivi Serikali itaweza kuishawishi Kampuni hii iweze kutoa huduma za usafiri wa anga katika miji ya Songea na Mtwara? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimesema kwamba, mashirika yote yanayofanya biashara ya usafirishaji wa abiria, yatakapotaka au kuonesha nia ya kwenda nchi ambazo tuna makubaliano nazo, Serikali itatoa ushirikiano kwa kufanya mazungumzo na kuhakikisha vibali vya kwenda katika nchi hizo vinatolewa.

Nia yetu mashirika yetu haya yaende nchi nyingi zaidi kadiri inavyowezekana kwa ajili ya kuwapa nafuu wasafiri wa nchi hii, lakini wao pia wana mambo yao ambayo wanayaangalia kabla ya kufikia uamuzi wa kuomba kwenda nchi moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Fastjet kwenda Miji ya Songea na kwingineko nchini, hili jambo pia linategemea na biashara inayopatikana katika maeneo hayo. Kwa sasa, kwa mfano, Fastjet hawana ndege ambazo zinaweza kwenda na kutua katika viwanja vingi vya mikoani hapa nchini, kwa sababu ndege hizi ni kubwa na zinaweza kutua katika viwanja vikubwa vitano

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

tu vilivyopo hapa nchini. Kwa hiyo, watakapoomba kufanya hivyo, sisi hatutasita tutawapa idhini mara moja.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Sanya, swali la nyongeza!

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mashirika ya Ndege ukiachana na Fastjet lakini Kenya Airways vilevile hutumia ndege aina ya Boeing 737; na ndege hizi lilitolewa agizo na Kampuni ya Boeing Marekani kwamba, nyaya zake za umeme hupita kwenye matanki ya mafuta na kila baada ya saa 50,000 za kuruka zinatakiwa ziwe *grounded* na kuwa *checked* kwamba waya hizi ziko salama hazijapata michubuko.

Je, Serikali yetu kupitia Wizara hii imefanya utafiti kwamba ndege hizo ambazo zina-*operate* Tanzania zina *certificate* ya kwamba baada ya saa 50,000 za kuruka zinafanyiwa uchunguzi kwa usalama wa abiria?

**SPIKA:** Ingawa swali ni jipya kabisa lakini kwa sababu wewe unahusika huko basi naomba ujibu!

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, idhini za ndege kuruka zinatolewa baada ya ndege hiyo na mmiliki wake na kampuni inayoiendesha kukidhi masharti ya Mamlaka yetu ya Usafiri wa Anga na masharti ya Shirika la Kimataifa la Usalama wa Anga (ICAO). Kwa hiyo, kama kuna jambo lolote linalohusu ndege ya aina fulani, taarifa hutolewa kwa Mashirika ya Usalama wa Anga Wanachama wote wa ICAO na ili ndege hizo ziweze kupata idhini ya kutumika katika nchi hizo, basi ni lazima masharti hayo yawe yametimizwa.

Vivyo hivyo, *Boeing, Airbus* na makampuni mengine na kama yatakuwa na jambo mahususi ambalo linahitaji kuangaliwa kwanza kabla ya kupata idhini, jambo hilo ni lazima lifanyike. Hapa kwetu mambo hayo yanafanyika na ndege zote zinazoruka hapa nchini zimepewa *Air Wealthness Certificates* ambazo zimeangalia mambo yote kama alivyouliza Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndassa!

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba; Shirika la Ndege la Tanzania sasa hivi linarusha ndege zake. Anaweza akatuambia ni ndege ngapi kwa sasa zinaruka?

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Uchukuzi, jibu kwa kifupi!

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndassa, kama ifuatavyo:-

Shirika letu la Tanzania la Air Tanzania sasa hivi linarusha ndege mbili; Dash 8 na CRJ Bombadia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee!

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Tunafahamu kwamba, Kampuni ya Fastjet ni kampuni ya kigeni, lakini vilevile tuna kampuni ya kizalendo ambayo inaonekana haifanyi vizuri kwa sasa, Kampuni ya Precision Air. Sasa nataka kufahamu kutoka Serikalini; kwa kuzingatia tuna-*encourage* Watanzania wawekeze ndani na *Precision* imeweza kufanya kazi kubwa na ikawa inatua kwenye maeneo ambayo hata *Fastjet* sasa hivi haiwezi kutua.

Serikali ina mipango gani ama ina mkakati gani wa kuweza kuisaidia Kampuni ya *Precision Air* ili itoke hapa ilipo na iweze kwenda mbele zaidi ukizingatia kwamba ATC imekufa au inasuasua?

**SPIKA:** Aah, basi bwana eeh, unaendelea tu! Mheshimiwa Waziri, majibu! (*Kicheko*)

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ambayo ameyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu Sekta hii ya Uchukuzi kwa njia ya ndege, naomba nijibu sasa swali la Mheshimiwa Halima Mdee, kuhusu Kampuni ya Precision.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilifuatwa na Kampuni ya Precision baada ya kupata matatizo makubwa ya *ki-operation*. Tumefanya kama tunavyotakiwa kufanya kama Serikali, lengo letu kubwa lilikuwa kufanya *intervention* lakini tumeshindana katika masharti. Kazi yetu sisi kwa kweli siyo *ku-risk u-private companies*, lakini pale ambapo inabidi tunafanya hivyo. Pale ambapo tunashindana kwa masharti hatuwezi kuendelea.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Ndege la Precision sidhani kama limefikia hatua mbaya ya *ku-collapse* na vilevile Mheshimiwa Halima Mdee, Air Tanzania haijafa, inaruka kwenda Mtwara, Kigoma, Songwe, Tabora, Mwanza, Arusha, Zanzibar, Bujumbura na pia Comoro. Mtu anayekufa haendi kote huko. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Aah, mbona mimi ya kufa sikusikia? Sasa tuendeleo na ratiba. Tuwatambue baadhi ya wageni tulionao. Mimi naomba ukimya maana watu wengine wamekuja hapa *just* kungea wanavyotaka, siyo hivyo. Waheshimiwa hapa, nawazungumza ninyi pia!

Wageni 13 wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Uwezeshaji, ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Katesh. Yuko Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Katesh, naomba asimame kama yupo na Wajumbe wengine pia wasimame. Tunawashukuru sana na karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Gerson Lwenge, ambao ni Mwenyekiti wa New Life in Christ Taifa, Reverend Canon Eliya Mkukuwala. Pia, yupo Mwinjilisti Daniel Shangali, ambaye ni Naibu Katibu Mkuu *New Life in Christ* Taifa; na yeye asimame alipo, ahsante sana tunashukuru. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane!

Kuna wageni wa Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, ambao ni Ndugu Mary Sure na Agness Kamili; naomba wasimame walipo. Ahsante sana. (*Makofi*)

Vilevile, kuna wageni 13 wa Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, kutoka Morogoro Kusini Mashariki, wakiongozwa na Ndugu Waziri S. Digalu. Naomba wasimame wageni hawa 13 popote walipo; ahsanteni sana na karibuni sana. (*Makofi*)

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Syvestry Koka, ambao ni Ndugu Godlisten Lyimo kutoka Marekani pamoja na Makatibu Kata kumi kutoka Jimbo la Kibaha Mjini, wakiongozwa na Ndugu Abdallah Mdimu, Katibu wa CCM Wilaya. Naomba wageni hawa wote wasimame. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Pia, kuna wageni wanne wa Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, ambao wanaongozwa na Ndugu Maximillian Chacha Matinde, Katibu wa Mbunge. Naomba hawa wageni wote wasimame. Ahsanteni sana.

Vilevile, kuna wageni wa Mheshimiwa Tundu Lissu, ambao ni wanafunzi 50 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Naomba wasimame wote popote walipo; ahsante sana lakini naomba msome vizuri. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Said Mtanda, ambao ni wanafunzi kumi kutoka Vyuo mbalimbali vya Mkoa wa Dodoma, wakiongozwa na Bwana Salum Hassan. Naomba na hapo pia wasimame mahali walipo; nadhani wamekosa nafasi lakini wanaweza kuwa ni hawa wengine. *(Makofi)*

Kuna wageni wetu wengine waliokuja kwa ajili ya mafunzo, nao ni wanafunzi 60 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Naomba wasimame, nadhani ni haohao. Tunawaomba msome kwa bidii. *(Makofi)*

Kuna wanafunzi 35 na Walimu wanne kutoka Shule ya Msingi Assumpter Moshi. Naomba wasimame; ahsanteni sana, tunawataka msome vizuri na mmependeza sana. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 50 na Walimu 17 kutoka Shule ya Msingi Kisiwani Dar es Salaam na hawa pia wasimame; ahsante sana Walimu kwa kuwaleta watoto na tunaomba pia wasome vizuri. *(Makofi)*

Matangazo ya kazi; Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa Deo Filikunjombe, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 8.30 kutakuwa na Kikao cha Kamati kwenye Ukumbi wa Msekwa C.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Rajab Mbarouk, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 7.30 watakutana na Ujumbe wa Nchi Wafadhili wa Bajeti ya Serikali (GBS) katika ukumbi wa Msekwa C. Tofauti ni nusu saa tu, lakini Ukumbi ni mmoja, mtajua wenyewe huko, labda ulikuwa ni mkutano mmoja lakini hamkuweza kuwasiliana.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret Sitta, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, mara baada ya kuahirisha kikao hiki, watakuwa na kikao chao katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Kwa hiyo, kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa mko watatu hapa, mtajua wapi mnakutana hukohuko.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea. Katibu hatua inayofuata!



## **UCHAGUZI**

### **Uchaguzi wa Wajumbe watatu wa Baraza ka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Uchaguzi wa Mjumbe mmoja wa Tume ya Utumishi ya Bunge**

#### **MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:** Mheshimiwa Wenje!

**MHE. EZEKIAH D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, wakati tunachangia Wizara ya Waziri Mkuu, Wabunge wa Dar es Salaam walizungumza sana, Mbunge wa Mwanza, Mbunge wa Iringa na hata Mbunge wa Mbeya, kuhusu suala la Wamachinga. Tulipozungumza tena kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Msigwa, alishika mpaka shilingi kuhusu suala la Wamachinga wanavyokuwa *treated* katika maeneo huko tunakotoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jibu lililotoka kwa Serikali ni kwamba, operesheni hizi za hovyohovy zilizokuwa zinaendelea kwenye haya maeneo, zitasitishwa kwanza ili Serikali ije na mpango mzuri wa namna gani tutakuwa tuna-*locate* Wamachinga hawa katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa ...

**SPIKA:** Ngoja tuelewane, hicho tunasema nini; mwongozo, maelezo binafsi au ni kitu gani?

**MHE. EZEKIAH D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, mwongozo wangu ninaoomba kwako ni kwamba, hivi sasa tunapozungumza hapa mabomu yanapigwa Mwanza kila kona na maduka yamefungwa, kwa sababu Wamachinga wanaondolewa na Polisi na bunduki na mabomu katika maeneo ya Makoroboi Mwanza.

Sasa nataka tu kujua *commitment* ya Serikali, zoezi hili lisimamishwe ili angalau ifanyike stadi nzuri ijulikane Wamachinga katika hii miji watapelekwa maeneo gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo mwongozo ninaouomba. (*Makofi*)

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona matumizi ya maeneno yetu humu ndani hayaeleweki, kwa sababu mimi huwezi kuniongoza mambo ya Serikali. Wewe ungetaka katika suala hili *fairly enough* ukatumia Kanuni ya 28 au 50, ungejieleza vizuri kwa sababu haya mambo yanakugusa wewe au eneo unalotoka.

Kwa hiyo, unatutaka sisi tueleze hao wanaohusika upande wa pili wasikie. Kwa sababu mimi sikumuagiza Waziri Mkuu wala nini, kwa hiyo bado ninakuagiza tumia Kanuni yetu ile ya 28 au 50 upate muda mrefu wa kueleza halafu tutaagiza wanaohusika wachukue hatua. Mimi sina mwongozo wala maelezo ya kukupa maana hakinihusu. Kwa hiyo, tunaendelea. Msimamizi wa Uchaguzi.

Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu maana kuna Waheshimiwa Wabunge wengine wanazurura katika ukumbi huu.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo kama Msimamizi wa Uchaguzi.

Waheshimiwa Wabunge, zoezi la uteuzi wa wagombea wa nafasi mbili, yaani Baraza la Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Tume ya Utumishi wa Bunge kama lilivyotangazwa tulipokea mrejesho tarehe 09 Juni na leo tarehe 11 Juni kama ilivyo kwenye *Order Paper* kutakuwa na uchaguzi wa Wajumbe watatu wa Baraza la Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kuziba nafasi zilizoachwa wazi baada ya muda wa Wajumbe waliokuwepo kumalizika.

Aidha, pamoja na uchaguzi wa Mjumbe mmoja wa Tume ya Utumishi wa Bunge kuziba nafasi iliyoachwa wazi na Mheshimiwa Godfrey Zambi aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia muda wa mwisho wa kurudisha fomu Jumatatu tarehe 09 Juni, 2014 saa kumi jioni Wabunge waliokuwa wamejitokeza kuchukua fomu na kuzirejesha ni kama wafuatao:-

Baraza la Chuo Kikuu Huria cha Tanzania waliochukua fomu ni Wabunge watatu ambao ni Mheshimiwa Dkt. Henry Dafa Shekifu, Mheshimiwa Sylvester Maselle Mabumba na Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa. Nafasi zinazotakiwa ni tatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge waliochukua fomu kugombea nafasi moja ya Tume ya Utumishi wa Bunge ni Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi na Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola.

Mheshimiwa Spika, kwa mamlaka iliyopo kwenye Kanuni nafasi za nasibu (*by election*) kwa nafasi ya Baraza la Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ni nafasi tatu, walioomba ni watatu, Wajumbe hao wamepita bila kupingwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni hayo sasa nitaeleza utaratibu wa uchaguzi wa nafasi ya Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge kwa maana ya nafasi moja.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 8(2)(b) ya Nyongeza ya Pili ya Kanuni za Bunge, wagombea nafasi ya Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge watatakiwa wafike mbele ya meza hii ili waweze kujieleza, kuulizwa maswali na kuyajibu na kisha kuomba kura.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Spika, baada ya kujieleza karatasi za kura zitatolewa ili kila Mheshimiwa Mbunge ambaye ndiye mpiga kura aweze kumpigia kura mgombea mmoja tu kwa kuweka alama ya 'v' na baada ya kupeleka kura yake katika masanduku ya kura kwa utaratibu utakaoelekezwa kura zitahesabiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni hayo narejesha kwako ili sasa zoezi la wagombea kujieleza liweze kufanywa kwa Wajumbe hao watatu kutoka nje na kuingia mmoja baada ya mwingine.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Haya ahsante. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kwanza niwapongeze wale Wabunge watatu, kinachoniridhisha ni kwamba kuna *gender*, kuna kila upande, *combination* ni nzuri, kwa hiyo, ninawapongeza wale wote. *(Makofi)*

Sasa tunaanza na utaratibu wetu wa kuwaita wale ambao tunatakiwa tuwahoji au mmalize kusema ninyi, halafu mimi nitasema baadaye. Eeh.

Kwa hiyo, kwanza kabisa ninaomba wafuatao waweze kutoka nje ili tuanze kazi. Tutawahoji kwa muda wa dakika tatu kama jana na wataulizwa maswali matatu kama yapo.

Wanaotakiwa kutoka nje sasa hivi ni Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi na Mheshimiwa Kangi Lugola. Hawa watoke nje, au wapo nje tayari? Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu atasogea mbele.

Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, mbele yako ni Waheshimiwa Wabunge ambao ndiyo watakaoamua hatima yako. Unapewa dakika tatu kujieleza na tutakuuliza maswali matatu kama yapo.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Waheshimiwa Wajumbe na Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama nilivyotamkwa Murtaza Ally Mangungu, Mbunge mwenzenu ambaye tupo pamoja hapa tangu kipindi cha mwaka 2010.

Waheshimiwa Wabunge, nina amini kabisa kila mmoja wenu ananifahamu vizuri, sina haja ya kujitambulisha kwa mengi lakini niwahakikishie kwamba nafasi ninayoimba ninaimudu na nitaweza kuwatumikia kama matakwa ya kisheria na kikanuni yanavyotamkwa, ahsanteni.

**SPIKA:** Swali Mheshimiwa Mkosamali.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa umesema utasimamia sheria na Katiba ya nchi inatamka kwamba uhai wa Wabunge ni miezi 60, utasimamiaje hali za Wabunge ndani ya miezi 60 ikiwa ni pamoja na malipo yao yote na mambo mengine? *(Makofi)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Nakushukuru sana.

**SPIKA:** Aah, ngoja nikuite Mheshimiwa Mangungu. Haya Mheshimiwa. *(Kicheko)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Nashukuru sana kwa swali lako.

Mheshimiwa Spika, kazi za Mbunge kama zilivyotamkwa kwenye masharti ya kazi za Mbunge, Mbunge anatakiwa apate stahiki zake zote kama zilivyoanishwa kwenye masharti hayo.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Kwa hiyo, nitahakikisha kama ilivyotamkwa kwenye sheria yenyewe ya uanzishwaji wa Tume ya Utumishi wa Bunge kuhakikisha kwamba kila Mbunge anapata kile anachotahiki na kwa wakati unaostahili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa mwingine, *balance*. Mheshimiwa Msigwa maana sijaona mwingine. Mheshimiwa Mchungaji.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Ndugu mgombea kuna mazoea na hulka iliyojengeka kwa watu wanaochaguliwa hawarudi kwa watu waliowachagua na kutoa mirejesho. Hata tuliokwishawachagua ambao unaziba nafasi toka tumewachagua hawajakaa na Wabunge ambao tumewachagua kuleta mrejesho wa namna gani watusikilize. *(Makofi)*

Wewe tukikuchagua ni namna gani utakomesha tabia hii ambayo haifai kwa mtu unayechaguliwa halafu hurudi kwa watu waliokuchagua ili kuondoa utaratibu uliokwishajengeka kwamba watu wakiishachaguliwa wanapotea, maana yake hata tuliowachagua huwa hawakai na sisi? Wewe utabadilishaje tabia hii?

**SPIKA:** Aah, hilo swali siyo sawasawa, ninayewarejeshea si mimi huwa ninaongea na ninyi kila siku kabla hatujaanza vikao? *(Kicheko/Makofi)*

Maana yake na mimi, kila siku tunapoanza vikao vya Bunge ndiyo mrejesho wenyewe. *(Makofi/Kicheko)*

Swali lingine Mheshimiwa Mtutura.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kwa kunipa fursa ya kumuuliza swali mgombea.

Mheshimiwa Mangungu kwa mwonekano wa juu juu unaonekana umri wako mdogo, lakini ukiangalia cv yako inaonekana una umri mkubwa, hebu lihakikishie Bunge hili kati ya sifa hizo mbili kipi ni cha ukweli? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Aah, mimi sasa sielewi. Mheshimiwa Mangungu. *(Kicheko)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumjibu muuliza swali kwamba muonekano wa mtu ni kutokana na maumbile aliyumbwa na Mwenyezi Mungu, kwa hiyo hiyo ni tafsiri yake na kula halali ndiyo kinachofaa zaidi.

**SPIKA:** Swali la mwisho kama lipo. Hakuna!

Mheshimiwa Mangungu ahsante, nakuomba uombe kura kabla hujaondoka.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naomba kura yako, Mheshimiwa Waziri Mkuu na viongozi wengine wote, Wabunge wenzangu wote naomba kura zenu niwatumikie, mnanifahamu vizuri, tunashirikiana katika kila jambo na Mheshimiwa Msigwa atathibitisha hilo kwamba siyo leo tu baada ya kura, kila siku tutaendelea kuwa pamoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**SPIKA:** Ahsante. Sasa tumuite Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi.

*(Hapa Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi aliingia Ukumbini)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, waliopo hapa ni Waheshimiwa Wabunge, tunakupa dakika tatu uweze kujieleza, baadaye tutakuuliza maswali matatu kama yapo.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Waheshimiwa sana Wabunge wenzangu, niliyesimama mbele yenu naitwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Jimbo la Bukene.

Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nimesimama hapa kwa heshima na tadhima kuomba mnipe kura zenu ili niwe Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge ili kwa kushirikiana na Wajumbe ambao tayari ni Wajumbe katika Tume hiyo tuweze kuboresha maslahi ya Wabunge na watumishi ambao siyo Wabunge ili Taasisi ya Bunge iweze kupata tija inayotarajiwa.

Waheshimiwa Wabunge, wote tunafahamu kwamba, tuna changamoto nyingi ambazo zinatukabiri kama Waheshimiwa Wabunge. Mbali ya changamoto iliyo wazi ambapo kwa sasa hivi hata zile stahiki zetu tunachelewa kuzipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, haikubaliki Waheshimiwa Wabunge kukaa zaidi ya siku 10 hawana posho ya kujikimu. Hili halikubaliki, linafanya Waheshimiwa Wabunge washindwe kutimiza kazi zao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, changamoto nyingine tuliyonayo ni kiwango kidogo cha mishahara ya Wabunge. Ninapozungumzia mishahara simaanishi *sitting allowance* wala *perdiem*, nina maanisha *basic salary*. Hasara ya kuwa na *basic salary* ndogo ni kwamba mwisho wa siku utapata *gratuity* ndogo, kwa sababu *gratuity* inapigiwa hesabu kwenye *basic salary*, siyo kwenye *sitting allowance* wala *perdiem*.

Mheshimiwa Spika, hasara nyingine ya kupata kiwango kidogo cha mishahara ni kupata *loan facility* ndogo. Taasisi za kibenki zinakopesha *based on basic salary*.

Waheshimiwa Wabunge, changamoto nyingine ambayo niko *determined* kuifanyia kazi....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mgombea)*

**SPIKA:** Kengele imegonga, dakika tatu zimeisha...

**WABUNGE FULANI:** Bado.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Waheshimiwa Wabunge, nipo *determined* kuboresha...

**SPIKA:** Heh, dakika tatu zimeisha. *(Kicheko)*

Maswali, rafiki zako wale wale wanauliza maswali, sasa nimruhusu Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Katika dakika tatu alizozitumia Mheshimiwa Zedi amezungumzia posho, mishahara na marupurupu. Kwa mtazamo wako wewe, kipaumbele cha Wabunge ili waweze kukuchagua ni

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

posho, mishahara na marupurupu kwa kuwa unaamini vilivyokuwepo sasa hivi havitoshelezi. Kwa hiyo, hicho ndiyo kipaumbele pekee?

**SPIKA:** Swali hilo.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Nashukuru sana kwa swali lako. Hayo niliyozungumza ni kutokana na muda jinsi ulivyokuwa, lakini nilikuwa na mengi. Kwa mfano, sasa hivi Waheshimiwa Wabunge kuna changamoto ya *interest* kwenye mikopo ambayo tunapata kutoka kwenye *financial institutions*. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, *financial institutions* zozote duniani *criteria* ya kwanza inayotumika kupanga *interest rate* ni *default rate* (kiwango cha watu ambao wanachukua mikopo na kutoroka bila kulipa).

Sasa katika Tanzania miaka miwili iyopita *default rate* ilikuwa 12% mpaka 15% lakini ukichukua Waheshimiwa Wabunge kama *segment default rate* is almost zero. Hakuna Mbunge ambaye anaweza kutoroka na mkopo kwa sababu ya udhibiti wa *ku-repay* ile *loan*.

Kwa hivyo, ili haki itendeke kwa mujibu wa taratibu za *financial institution*, *market segment* ambayo *default rate* ni zero, *interest* yake ni very low. Kwa hiyo, *interest rate* ambayo tunatozwa Waheshimiwa Wabunge ni kubwa mno kwa sababu sisi *default rate* yetu is almost zero. (Makofi)

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Haroub.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mheshimiwa mgombea swali moja tu.

Mheshimiwa mgombea pamoja na mambo uliyoyataja ya kuwatetea Wabunge lakini pia katika Bunge hili kuna changamoto ya Bunge kutofanya kazi kama Bunge. Bunge linafanya kazi kwa mtazamo wa vyama na hii inasababisha Bunge letu kudharaulika na kukosa sifa nje katika taasisi za kimataifa kama ripoti ya *Transparency International* ilivyoeleza kwamba Bunge hili halina sifa kwa sababu halifanyi kazi kama Bunge kutetea wananchi, lakini linafanya kazi kutetea vyama vyao zaidi.

Je, changamoto hii tukikuchagua wewe katika nafasi hiyo utasaidia vipi kulitatua?

**SPIKA:** Aah, siyo swali lake hili, kwa sababu Tume haifanyi kazi ya kulisimamia Bunge, inasimamia huduma za Wabunge. Kwa hiyo hilo siyo swali linalohusu huduma za Wabunge. Mheshimiwa Said Mtanda. (Makofi)

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niweze kumuuliza Mheshimiwa Zedi swali dogo.

Nimekuwa Mbunge hapa kwa miaka takribani sasa mitatu na nusu kuelekea minne, lakini jimbo langu halina Ofisi ya Mbunge na sina mtaalam mwelekezi wa kunisaidia katika kutengeneza mipango ya kuhakikisha kwamba ninafanya kazi zangu vizuri kitaaluma. Ninataka nifahamu ukiwa Kamishna wa Bunge suala hili la Wabunge kutokuwa na ofisi za kudumu kwenye majimbo yetu utalichukulia hatua gani? (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Zedi majibu.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Nashukuru sana Mheshimiwa Mtanda kwa swali lako zuri.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Kati ya mambo ambayo mkinichagua leo kuingia kwenye Tume ya Utumishi wa Bunge ambalo nitalisimamia kwa nguvu zote ni kuhakikisha Ofisi za Bunge zinakuwa kamili kwa maana ya utimilifu wake kuhakikisha kwamba tija inapatikana.

Waheshimiwa Wabunge, kuna jambo moja ambalo ni muhimu sana, ili Wabunge tuweze kutunga sheria au kufanya maamuzi, tunahitaji kusoma *documents* nyingi sana.

Kwa hiyo, jambo la kwanza ambalo nitafanya kuhakikisha ni kwamba pamoja na *infrastructure* za ofisi kama jengo, *furniture* na nini, lakini Wabunge tuwe na wasaidizi wanaotambulika na Bunge ambao wana uwezo wa kitaaluma wa kufanya tafiti, kuchambua *information* na kumrahisishia Mbunge kwa kuweka katika *summary* ambayo Mbunge ndiyo atachukua na kuweza kufanyia maamuzi.

Sasa hivi Wabunge tuna *documents* nyingi na makabrasha mengi ambayo kwa vyovyote muda wa kuyasoma yote haiwezekani.

Kwa hiyo, nitakachopigania ni kuhakikisha kwamba Wabunge tunakuwa na msaidizi anayetambulika na Ofisi ya Bunge, lakini ana uwezo wa kufanya tafiti, kuchambua mambo na kuhakikisha kwamba Wabunge tunarahisishiwa kuwa na *information* ambazo zitatusaidia kufanya maamuzi.

Kwa hiyo, ofisi ni *priority*, lakini kwa maana ya ofisi kukamilika, *infrastructure* za kiofisi, jengo, *furniture*, lakini kuwa na wasaidizi ambao watafanya Mbunge awe kama kaatasisi kadogo ambako kamekamilika na ili tija ya Mbunge iweze kupatikana kama ambavyo inatarajiwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii. Eeh, Mheshimiwa Sophia umeahirisha, sijui! Basi tunaendelea.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Napenda kumuuliza mgombea kwamba katika kipindi hiki chote sisi Wabunge wa Viti Maalum tumekuwa tuna matatizo kidogo hasa kuhusu kule majimboni kutoa misaada kwa vile ile *catalyst fund* hatupati. Sijui utazungumzije hilo huko kwenye Kamisheni? *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa jibu.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa swali lako zuri sana.

Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum nawaombeni mnipe kura zenu kwa sababu hiki ni kilio kikubwa sana. Ni kweli kabisa Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum mnatoa huduma kwa kiwango kikubwa sana na kwa kimsingi jimbo lenu ni mkoa mzima, ukubwa wake unazidi hata Mbunge wa Jimbo moja. Kwa hiyo mna kila sababu ya kusaidiwa kuwa na *catalyst fund* ambayo itawawezesha na ninyi pia kule mnakopita muweze kuchangia nguvu za wananchi.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum naomba mniunge mkono, hoja yenu ni ya msingi sana na inahitaji kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa sasa omba kura maswali matatu yamefika.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Waheshimiwa Wabunge wenzangu nipo *determined* kusaidiana

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

na Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge waliopo sasa hivi kuhakikisha tunaleta mabadiliko katika mambo yote yanayohitaji ili ufanisi wa Taasisi ya Bunge uwe na tija inayotarajiwa na wananchi wetu.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kura zenu zote. Ahsanteni sana.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Zedi.

Sasa aitwe Mheshimiwa Kangi Lugola. *(Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola aliingia ukumbini akiwa amevaa bango lenye maneno ya kuomba kura)*

**SPIKA:** Haya msikilizeni, naomba msikilizeni, haya Waheshimiwa tutulie sasa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola hawa ni Waheshimiwa Wabunge, tunakupa dakika tatu kujieleza na baadaye maswali matatu ikibidi.

### **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni zetu tuna mavazi maalum ya Kibunge. Nilitaka kujua kama hii ni kitu sawa sawa. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Sasa hii sio sawa sawa. Hiyo sio sehemu ya mavazi ya Bunge tunaomba utoe. Tunaomba uitoe. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola alivua bango alilokuwa amevaa)*

**SPIKA:** Nakupa dakika tatu, naomba tuendeleo hivi sasa.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba samahani sikujua kama mabango kama kipeperushi hayaruhusiwi humu ndani. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge mimi naitwa Kangi Lugola, tumekaa sote hapa miaka minne sasa, naamini tunafahamiana kwa tabia na kwa uwezo.

Waheshimiwa Wabunge nisingependa nichukue muda wenu mwingi naomba mnichague kura zote kabisa ili niwe Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba mtutazame usoni tunaposema tutawatetea mkitutazama usoni mjue kweli huyu anamaanisha. Isije ikawa kama porojo na blaa blaa tukishasema hapa tunaachana hapa hapa.

Kwa mujibu wa Katiba hii Wabunge maslahi yetu yanafahamika. Nitakuwa mtetezi mpaka jasho langu la mwisho kuhakikisha kwamba stahili zote za Wabunge kwa mujibu wa Katiba, nitakuwa tayari nikishirikiana na wenzangu kuwashawishi tushinde ikibidi Ikulu tukitembeza bakuri kwa ajili ya maslahi na kulinda Katiba hii. *(Makofi)*

Nitashirikiana na wenzangu kuhakikisha kwamba hata kama *penalty* haikabwi tunaikaba ili sheria hii ya Bunge inayohusu maslahi ya Wabunge, inayohusu maslahi ya watumishi yako humu kupandishwa vyeo, kuthibitishwa lazima mimi kauli yangu ninaisema kwenu lazima nitakuwa mtetezi wenu wa kweli na wa dhati na mnanifahamu. *(Makofi)*



## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Sisi Wabunge ndio macho, ndio masikio, ndio mdomo, ndio pua ya wapiga kura wetu. Tunahitaji Tume ya Utumishi ya Bunge ambayo ni *strong* ili tuweze kuthibitisha kwamba kweli Bunge hili linakuwa na afya, Wabunge wanakuwa na afya na watumishi wanakuwa na afya. Tusije tukafika pahali tukakubali porojo hapa tukatoka Wabunge hapa tukiwa na utapiamlo. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Dakika tatu zimefika, swali. Sasa nimuite Mheshimiwa nani. Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Kaeni basi, kaeni bwana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan huna sababu ya kuagiza wenzio wenyewe watakaa.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa mgombea kwa muda mrefu sana Wabunge wa Viti Maalum tumekuwa tukidai fedha za jimbo lakini kwa muda mrefu sana na wewe ukiwa humu ndani ya Bunge umekuwa ukilisikia. Kama tutakuchagua au kama utachaguliwa utawahakikishiaje akinamama ambao ni asilimia 37 ya Wabunge wote kwamba wataenda kufaidika na mfuko huo hasa ikizingatiwa kwamba akinamama hawa wanawakilisha eneo kubwa sana, wengine ni mikoa lakini wengine ni Taifa kwa ujumla wake.

Je, utatuhakikishiaje kwamba unaenda kutetea maslahi ya Wabunge wanawake ili waweze kufaidika na mfuko huu?

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Lukuvi.

**SPIKA:** Mheshimiwa ahaa! Mheshimiwa tunaitwa kwanza sio kusema tu. Haya Mheshimiwa Lugola.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Lukuvi tumekuwa Wabunge tukiomba mambo mbalimbali hapa anasema Tume ikikaa itaifanyia kazi. Hapo ndipo mjue umuhimu na unyeti wa Tume ya Utumishi wa Bunge na hata jana suala la ulinzi na usalama suala la Tume. Sasa Tume inahitaji mtu kama mimi ambaye ninapiga vita mfumo dume katika Bunge hili kwa sababu kwa mujibu wa sheria hii ya Bunge Tume hii ina mamlaka na uwezo wa kuangalia namna gani katika uendeshaji bora wa Bunge na Majimboni kule tunaweza tukawa na ustawi. (Makofi)

Kwa hiyo mama yangu Mheshimiwa Lyimo ukinichagua mimi na Mheshimiwa Spika yupo hapa ndiyo Mwenyekiti wetu wa Tume nadhani nitahakikisha naanza kumuomba ili tuanze kuorodhesha mambo ambayo sisi Wabunge tunahitaji tuyatatue kwenye Tume katika kipindi hiki.

**SPIKA:** Ahaa, Mheshimiwa Hussein.

**MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja.

Mheshimiwa Kangi katika miaka 1960, 1970 na 1980 katika miiko na maadili ya viongozi kulikuwa na utaratibu ulikuwa unasema au *slogan* inasema kwamba kiongozi anatakiwa awe

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

mfano mzuri kwa tabia yake na vitendo vyake. Je, unaweza ukatupa mifano michache wa uongozi wako wa tabia zako na vitendo vyako vipi ulifanikiwa? Nashukuru. *(Kicheko)*

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Cha kwanza ambacho lazima nikionyeshe ni ile tabia yangu ya kuwa mkweli. Nitahakikisha Tume hii ambayo ni chombo muhimu inafanya kazi za kuhakikisha kwamba ukweli kuhusiana na maslahi ya Wabunge kwa mujibu wa Katiba na stahili zingine na watumishi lazima ukweli ujulikane.

Lakini la pili, mimi ni mtu jasiri, lazima nidhihirishe ujasiri wangu katika ile Tume ya Utumishi. Katika kudhihirisha niliwahi kusema pale kwenye *briefing* kwamba Tume yetu hii tuliyoichagua tunaitaka angalau tunapokuja Bungeni pamoja na kwamba Mheshimiwa Spika ndio Mwenyekiti wa Tume, Tume ile basi tuone ikiwa imekaa pale mbele ili iweze kuwajibika kwetu sisi kama kuna mambo ya kuwauliza tuwaulize, kama kuna mambo ya kuwasaidia kama *inputs* tuwasaidie. *(Makofi)*

Kwa hiyo nitatumia ujasiri ule kumshawishi Mheshimiwa Spika kwamba ni wakati muafaka sasa lazima Tume hii twende mbele ya Bunge. Lakini lingine ambalo mimi *professionally* mnanifahamu, ni mwanausalama. *(Makofi/Kicheko)*

Kitu kimoja ambacho nitahakikisha kwamba tunakifanyia kazi ili kuonyesha taaluma yangu na nikiwa Bunge la Afrika Mashariki tumetembelea Mabunge mengi ya wenzetu, mimi nimefanya *attachment* nyingi kwenye Mabunge, nimeshuhudia kwa macho yangu Wabunge wana ulinzi kwa sababu ya *venerability* ya Mbunge. *(Makofi)*

Kwa hiyo, suala hili lazima la lenyewe nionyeshe hiyo *professionalism* yangu katika Tume. Kwa hiyo yapo mambo mengi kwa sababu ya muda lazima yatadhihirika kwamba huyu ndiye Kangi Lugola mnayemfahamu. *(Makofi)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, Mabunge yaliyopita katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba inasema kwamba maisha ya Bunge ni miezi 60, lakini Bunge lililopita mishahara iliyolipwa katika Bunge lililopita haikufikia miezi 60. Tume ilikuwepo na Katiba inasema lakini hatukulipwa miezi 60. Lakini tunajua kwamba kama shida itatokea baada ya Bunge kuahirishwa, Bunge lile la mwisho Bunge linaweza kuitwa wakati wowote kwa ajili ya shughuli maalum. Lakini hilo halikufanyika kwa kipindi kilichopita katika Bunge lililopita.

Sasa namuuliza Mheshimiwa mgombea kwamba utatusaidiaje kukamilisha miezi 60 ya *life span* ya Bunge? *(Makofi)*

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Kwanza kabisa Bunge hili Bunge la Tisa limeishang'atwa na nyoka. Hawakuweza kupata stahili zao kwa mujibu wa Katiba hii, Ibara ya 65 inatamka wazi kuwakumbusha tu Waheshimiwa Wabunge; "Bila ya kuathiri masharti mengineo ya Katiba hii maisha ya kila Bunge yatakuwa ni muda wa miaka mitano." Miaka mitano ni miezi 60. Kwa sababu tumeshang'atwa na nyoka nitatoa mchango wangu wa hali ya juu kwa kumsaidia Spika na Wajumbe wenzangu na hili kwa kweli ndilo kwangu mimi hii ndio kipaumbele namba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhakikisha kwamba tunaanza maandalizi mapema kwenye Tume yetu ili tutakapokuwa tunatoka mwezi Juni hapa na hata hii sheria ya Bunge inasema wazi kabisa kwamba tutakapokuwa Bunge limevunjwa, Tume itaendelea na kazi mpaka Bunge lingine litakalokuja. Huu ndio ushahidi kwamba Tume bado iko kazini kuhakikisha kwamba mambo yenu haya miezi minne mtayapata na yanawafuata huko Majimboni mliko. Kwa hiyo,

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

msiwe na wasiwasi kama ni Kamishna kwa kweli mmepeata. Kama ni Kamishna kwa kweli huyu ndiye Kamishna huyu. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante maswali matatu yamefika. Maswali matatu tayari sasa omba kura zako sasa.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima ninaomba kura, najua hapo ulipo unaweza ukaandika vi-note unaniombea kura huku. Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kura, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni naomba kura, Waheshimiwa Wabunge wote bila kujali itikadi zetu, bila kujali itikadi zetu, bila kujali itikadi zetu ninaomba kura kwa heshima na taadhima na hii kazi niweze kuianza leo kwa kumwomba Spika aitithe kikao cha kwanza tuanze kazi. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Haya ahsante Mheshimiwa Lugola. *(Makofi/Kicheko)*

**MJUMBE FULANI:** *Big Results Now.*

**SPIKA:** Haya tunashukuru msimamizi wa uchaguzi. Msingekosa kucheka basi muwe na watu wa namna hiyo pia. Haya tunaendelea. Naomba tusikilize.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, baada ya zoezi hilo kukamilika naomba kutoa utaratibu wa namna ya zoezi la kupiga kura litakavyoendeshwa.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo tutatoa karatasi ya kura kwa kila Mbunge na utajaza karatasi hiyo alama “v” kwa kuchagua jina moja kati ya majina matatu.

**SPIKA:** Waheshimiwa naomba tusikilize basi.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Tutatoa karatasi ya kura ambayo tutaomba Waheshimiwa Wabunge hapo mlipo mpokee na mpige kura lakini utaratibu wa kuja kutumbukiza karatasi ya kura utafanywa kwa utaratibu kwamba upande mmoja wa kulia na kushoto, mstari wa kwanza na wa pili na kuendelea watakuwa wanakuja kwa utaratibu kuweka karatasi za kura mbele ya meza ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba sasa tulete masanduku na pia tugawe karatasi za kura.

*(Hapa karatasi za kupigia kura ziligawiwa)*

**SPIKA:** Karatasi za kura ziko wapi? Mgawie kila mtu apewe mkononi karatasi moja, sio mnahesabu mnagawa. Sio kuhesabu kama unavyofanya wewe sivyo.

*(Hapa karatasi za kupigia kura ziligawiwa)*

**SPIKA:** Mtu anapewa karatasi mkononi sio mnahesabu mnagawa. Waheshimiwa, tunajua kuandika kila mtu anaweza kuandika maneno maneno ya kazi gani.

Hebu nyanyueni maboksi yenu, yapo wapi maboksi? Nani anayehusika? Pale page people yako wapi maboksi.

**SPIKA:** Kuna tatizo? Ilikuwa je? Alimpaje Kura? Hamrudishi kura mtakuja kuziweka wenyewe hapa, aliyechukua amepeleka wapi? Kaitafute ile karatasi na thibitisha iko wapi.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Tunaanza kurudisha na *block* hii hapa na *block* hii hapa kwa upande huu. Waliweka wapi hiyo karatasi mnayosema? Aah!

Waheshimiwa Wabunge, mnapofanya shughuli nendeni kimya jamani kelele nazo ni sehemu ya vurugu. Jamani mistari mingine ingekuwa inatembea kungekuwa hakuna mbanano hapo tafuteni njia ya kutembea. Pia naomba Mheshimiwa Lowassa hilo kundi hapo libomoke.

Waheshimiwa kama wote mmerudisha karatasi zenu, sasa ninaomba watoe Mawakala au wao wenyewe waende Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, tafadhali naomba tu-*close* hili zoezi, sielewi kwa nini mtu anaweza kuwa peke yake nyuma mlikuwa wapi? Mheshimiwa Ally Mangungu.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Hillary Aeshi aniwakilishe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aeshi sokea mbele. Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi ni nani anakuwakilisha?

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, nitakwenda mwenyewe.

**SPIKA:** Sokea mbele, Mheshimiwa Kangi Lugola?

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Deo Haule Filikunjombe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo asogee. Haya msimamizi wa uchaguzi na watu wako mwende huko. Mheshimiwa Filikunjombe unatakiwa kwenda na wenzako utakwendaje peke yako baadaye? Ala!

Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya kutumia vizuri muda huu, naomba nimwite Mheshimiwa Mwakyembe, kulikuwa na suala lililohusika na mambo ya ndege inayoruka kule. Mheshimiwa Mwakyembe sokea hapa, ni taarifa ya Serikali!

*(Hapa kura ziliendelea kuhesabiwa)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na Mwongozo ulioombwa na Mbunge wa Ileje Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona kwako Mheshimiwa Spika, jana tarehe 10 Juni, 2014 kuhusu ndege ambazo kwa siku kadhaa wananchi wanaoishi mpakani na Malawi wameziona zikivinjari karibu na maeneo yao na ukaitaka Serikali kutoa ufafanuzi. Naomba sasa kwa ruhusa yako, nitoe ufafanuzi ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Kibona kwa taarifa yake ya jana na kuwashukuru wananchi wote wa mpakani hasa Wilaya za Ileje na Kyela kwa kutoa taarifa haraka kwa viongozi wa Wilaya zao mara baada ya kuingiwa na wasiwasi kuhusu ndege hizo.

Mheshimiwa Spika, ulinzi wa Taifa letu unategemea kila mmoja wetu. Naomba nitoe taarifa kuwa Serikali imejiridhisha kuwa ndege ambazo zinaonekana mpakani mwa Tanzania na Malawi ni ndege maalum za utafiti ambazo vyombo vyetu vya udhibiti wa anga zimezipa vibali vya kuwa maeneo hayo na vinaziona na kufuatilia mwenendo wake kwa karibu. Kama nilivyokwisha sema ni kwamba, Serikali imejiridhisha kuwa, hakuna ndege zingine zaidi ya hizo za utafiti katika eneo hilo la nchi.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Spika, kilichokosekana hapa ni taarifa sahihi ndani ya muda muafaka kwa wananchi kuwa wategemee shughuli za kiutafiti wa aina hiyo katika maeneo yao. Aidha, Wizara imeisitizia Mamlaka ya Usafiri wa anga TCAA kuhakikisha kuwa mara zote wananchi kupitia viongozi wao wa Mikoa na Wilaya wanapewa taarifa mapema kuhusu shughuli za aina hiyo katika maeneo yao ili kuepusha taharuki na hali ya wasiwasi inayoweza kujitokeza miongoni mwao.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha kuelezea ndege tatu maalum za utafiti siyo C-GSGJ Cessna 208 C-GSGJL Cessna 280 na C-GSGL Type 280 zinafanya kazi ya kukusanya takwimu za kijiolojia nchini Malawi na zina vibali vyote vya TCAA kuruhusu ndege hizo zinazoruka chini chini zikifanya kinachoitwa *Low Level Survey* kugeuzia ndani ya Tanzania lakini siyo zaidi ya 10 NM yaani *Nautical Miles* kumi. Ndege hizo zinapogeuzia Tanzania haziruhusiwi kabisa kukusanya takwimu zozote za kiutafiti, ni kugeuza tu.

Mheshimiwa Spika, ndege zote tatu ni za kampuni ya *Sander Geophysics Tanzania Limited* ya sanduku la posta 903 Dodoma. Makao Makuu ya kampuni hii yako Ottawa Canada, awali ndege hizi zilitekeleza mradi wa kupiga picha na kukusanya takwimu za kijiolojia nchini Tanzania katika mradi wa Wizara ya Nishati na Madini ambao ulitekelezwa kwa kutumia fedha za Benki ya Dunia kipindi cha mwaka 2011/2012 na mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, baadaye kampuni hii ilishinda sabuni nyingine nchini Malawi vile vile chini ya Ufadhili wa Benki ya Dunia, lakini utekelezaji wa mradi huo uliahirishwa mpaka mwishoni mwa Mei na mwanzo wa Juni mwaka huu kutokana na hali ya hewa kutokuwa nzuri katika eneo hilo la Ziwa Nyasa kwa kazi ya aiana hiyo ya utafiti.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuwatia moyo wananchi waendeleo na moyo huo huo wa Uzalendo na wa Kitaifa wa kutoa taarifa mapema kwa vyombo vya dola yanapotokea matukio yasiyo ya kawaida katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha ufafanuzi huo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha asubuhi baada ya kipindi cha maswali Mheshimiwa Wenje alikuwa ameomba Mwongozo kwa jambo ambalo nilimuagiza kwamba atumie kifungu cha (28) au kifungu cha (50) kuweza kuleta maelezo binafsi, lakini baada ya kutafakari kwamba leo tarehe 11 tutaahirisha kikao hiki baada ya kutoa matokeo na kesho siku ya bajeti maana yake nikimwambia hivyo ni kwamba hili lihusike siku ya Jumatatu ijayo. Kwa hiyo nimeona ni bora nibadilishe uamuzi wangu nimruhusu atumie kifungu cha (47)(1) atoe maelezo kwa dakika tano, halafu nitaendesha kikao. Mheshimiwa Wenje!

**MHE. EZEKIAH D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Hoja niliyonayo ni kwamba, muda huu tunapokaa hapa Bungeni Jiji la Mwanza kumechafuka, mabomu yanapigwa kila kona na maduka yote yamefungwa kati operesheni ya kuondoa Machinga katika eneo la Makorobo.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba operesheni ya namna hii mwaka 2011 ilifanyika kwa *involve* Polisi, kuna maisha ya watu yalipotea Mwanza. Mwaka 2012 Operesheni kama hii pia ilitokea na kuna watu walipata ulemavu wa kudumu mpaka leo. Natambua kwamba suala la Wamachinga limekuwa ni suala Kitaifa Mbeya kuna tatizo, Dar es Salaam kuna tatizo, Mwanza kuna tatizo, Iringa kuna tatizo, Arusha kuna tatizo, miji yote kuna tatizo na ndiyo maana kwa uzito wake kipindi cha bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara Wabunge wengi walizungumzia hili suala.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

Mheshimiwa Spika, nakumbuka Mheshimiwa Msigwa alikwenda mbali mpaka akashika shilingi ili utoke msimamo wa Serikali Kitaifa kuhusu namna gani ya kushughulikia masuala ya Machinga.

Mheshimiwa Spika, kwa hili linaloendelea Mwanza leo, maduka yoye yamefungwa, biashara zote zime-collapse Mwanza ambapo hizo biashara ndiyo zinafanyika ili Serikali ipate kodi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kupitia kiti chako, Serikali iagize hiyo operesheni inayoendelea Mwanza isimame, halafu Serikali ya Mkoa wa Mwanza na maeneo mengine nchini kama Serikali ilivyotoa *commitment* kwenye Bajeti ya Wizara, Viwanda na biashara ikae na itafute ufumbuzi wa kudumu kwa masuala ya wafanyabiashara ndogondogo kwa sababu ni tatizo la nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa kiti chako naomba Serikali isitishie hili zoezi Mwanza kwa sababu inakwenda kugharimu mpaka maisha ya watu, ikiwezekana tujadili kwenye Bunge ili tupate ufumbuzi wa kudumu kwa sababu hili ni tatizo la nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia Kanuni ya (47), naomba kutoa hoja ili hili suala lijadiliwe hata kwa kifupi.

**SPIKA:** Sasa watu wanasimama jamani eeh! Kifungu ni cha (47)(1) suala la dharura, kwa sababu asubuhi alishasema, kwa hiyo mazingira ya hoja ile nilishaelewa kwamba inahitaji maamuzi hayo, ndiyo maana nimempa ruhusa moja kwa moja ajieleze kwa muda wa dakika tano. Sasa naitaka Serikali ieleze, katika suala hilo la Mwanza. Hii habari nyingine ni hoja ndefu ya Machinga mtazungumza mkipenda Mheshimiwa Waziri Mkuu au mtu wako anayejuu! (Kicheko)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba jambo hili lilitolewa humu ndani na bado Serikali inakusudia kutoa taarifa kama tulivyoahidi, tumetoa maelekezo, tunaandaa taarifa juu ya suala hili la Machinga na tutakuja kulitolea hapa Bungeni.

**SPIKA:** Mheshimiwa tuwe pamoja tunazungumzia asubuhi...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Ndiyo nakuja hiyo ya Mwanza sasa.

**SPIKA:** Naomba ukae.

Hili hatukutolea uamuzi, mimi ndiyo niliyemsimamisha huyu. Sasa tusiwe tunazungumza kitu kingine, tunazungumza hiki anachokisema Wenje cha Mwanza, siyo habari ya Machinga wa nchi nzima, ni cha Mwanza kinachoendelea sasa, kama kinaendelea, Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nataka kutoa taarifa, naanza toka mwanzo lakini hii taarifa ya Mheshimiwa Wenje Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoka hapa amekwenda kuzungumza na wahusika, tutachukua hatua kwa issue ya mwanzo, tunatafuta ukweli wa hali halisi, lakini hatuwezi kusimamisha kwa kauli hapa. Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuja kupiga kura, anaendelea kufanya mazungumzo kujua ni kitu

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

gani kinaendelea huko Mwanza, kwa sababu masuala ya *Law and Oder* yanaendelea mahali kote, ni jukumu la Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Wenje kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshaanza kulishughulikia hili na amekuja tu kupiga kura na anaendelea kulishughulikia hili jambo litakwenda vizuri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo dogo...

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea  
na Spika kuonesha wakitaka kujadili hoja ya  
Mheshimiwa Wenje)*

**SPIKA:** Kanuni someni, Spika ana Mamlaka ya kuamua ni kiwango gani cha watu watajadili, sasa nimeshamaliza.

Kwa hiyo, tunaendelea Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Cecilia Pareso, kwa niaba ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Selasini anasema kwamba, saa saba lbada ya wale wa Kanisa Katoliki pale juu ipo leo. Kwa hiyo, naomba uvumilivu wenu ili kusudi tuweze kupokea matokeo.

*(Hapa Kura ziliendelea kuhesabiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuchukue nafasi hii tukumbushane kesho ndiyo *Budget Day*. Asubuhi tutakuwa na kipindi cha Maswali kama kawaida. Baada ya kipindi cha Maswali, Waziri wa Nchi anayehusika na mambo ya Mpango atasoma Mpango wa Nchi asubuhi. Akishamaliza kusoma tutaahirisha kikao asubuhi ile, lakini tutarudi tena saa kumi, sio saa kumi na moja ndiyo kawaida za *Budget Day* zote.

Ni kwa sababu siku hiyo saa kumi, wenzetu pia katika maeneo ya Afrika Mashariki watakuwa wanasoma wakati ule ule, kwa hiyo, saa kumi tunarudi hapa kumsikiliza Waziri wa Fedha. Akimaliza kusoma hotuba yake, siku ya tarehe 13 hatutakuwa na Bunge ambayo ni siku ya Ijumaa, pia Jumamosi tarehe 14 hatutakuwa na Bunge na tarehe 16 tutaanza kujadili ile hotuba.

Sasa nawakumbusha wote ambao hawajaomba kujadili ile hotuba, waombe kwa sababu tutaingia katika mpango ule ule wa dakika zile zile kuona kwamba tunajadili kufuatana na uwiano unaostahili. Kwa hiyo, mkileta maombi pale tutapanga namna na jinsi watu watakavyokuwa wanaongea. Kama kawaida hotuba ya Bajeti ni ya jumla unazungumza chochote hubanwi na eneo fulani maalum kwa sababu pale kutakuwa na Mpango na Bajeti yenyewe.

Kwa hiyo, nadhani maombi mtayapeleka Ofisi ya Bunge kusudi muweze kupanga wanaoanza Jumatatu na siku zinazofuatia. Kwa hiyo, mzingatie hivyo na kawaida kama tutatumia dakika zetu zile, karibu wote mtapata nafasi za kujadili hotuba ile.

**WABUNGE FULANI:** Tumeshajaza.

**SPIKA:** Mmeshajaza?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**SPIKA:** Basi zitapangwa watakavyoona inafaa. Kwa dakika zetu saba mnaweza kujadili wengi sana, kwa siku tano. Msubiri kidogo matokeo yanakuja! Tutatumia zile fomu na wengine ambao hawajajaza tunawakaribisha, lakini tutatumia ile kama *priority* namba moja.

Mheshimiwa Paresso analikaribisha lile suala, tulidhani kwamba Bunge litaisha saa saba anasema ile ibada inaanza saa sita na nusu badala ya saba, kwa hiyo, naamini kabla ya saa sita tutakuwa tumemaliza kazi hapa. Saa sita na nusu wanaokwenda kusali hapa juu.

Nawaambia Mawakala waache ushabiki wao, Filikunjombe nenda kakae mahali pako. *(Kicheko)*

Sisi siku moja, sikilizeni! Siku moja tulisimamia uchaguzi fulani, hii ya kusema kwamba nakwenda kusimamia mwenyewe, basi mtu mmoja akaenda kusimamia mwenyewe. Alipofika kule akawa ameanguka kibao, sasa akalia, ikabidi tukae saa nzima analia tu. Alipomaliza kulia tukamwambia ufute machozi na upite mlango wa nyuma uende. Basi wakaenda kwenye baa kunywa pombe, mwenzake homa, akaona huyu anafurahi bila shida! Siku ya kutangaza akashangaa yeye ndiye aliyeanguka aliyekwenda huko.

Kwa hiyo, siyo kwamba itatokea hivyo leo. Kwa hiyo, nashukuru sana kwa kazi mliyofanya, lakini niwashukuru nyie kwa utulivu wenu, wakati tunasubiri hakuna hata aliyeamua kwenda kunywa chai kwa sababu Waheshimiwa hao wameshatoa matumaini mazito mazito, sasa badala ya kuuliza Tume nzima, saa nyingine mtamuuliza Mbunge mmoja mmoja, Mjumbe wa Tume aliyeahidi anafanyaje!

*(Hapa Matokeo ya Kura Yalitangazwa)*

Waheshimiwa Wabunge kura zilizopigwa 235, idadi ya kura zilizoharibika ni moja, neno kuharibika, sijui maana yake. Matokeo ya kura ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi amepata kura 46, Mheshimiwa Murtaza Mangungu amepata kura 61, Mheshimiwa Kangi Lugola amepata kura 127. *(Makofi/Vigelegele)*

Kwa hiyo, namtangaza Mheshimiwa Kangi Lugola kuwa ndiye Mjumbe mpya wa Tume ya Utumishi wa Bunge. *(Makofi/Vigelegele)*

Kwa utaratibu wetu Mheshimiwa Selemani Zedi aje ajieleze. Hakuna uhasama hapa tunazungumza tu. Mheshimiwa Zedi! Dakika tatu!

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naomba kuchukua fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa kura ambazo mmenipatia ambazo zinaonesha kwamba mnaimani na mimi na kwamba huu siyo mwisho kwa sababu nafasi ilikuwa moja, ni lazima apatikane mmoja, lakini mbele ya safari nafasi zitakuwepo, naamini uwezo wangu mmeuona na naamini nafasi zitakapokuwepo mtanipatia.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zedi. Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu!



## **Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na zaidi niwashukuru Wabunge wenzangu wote ambao waliweza kunipigia kura. Kwa kuwa mimi ni mtu ambaye namwamini sana Mungu nasema kwamba jitihada haishindi kudra.

Nawashukuruni sana na niwahakikishie tutaendelea kuwa wamoja, tutashirikiana kwa kadri ya kiasi ambacho Mungu atatuwezesha. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutoa kibali mimi kuwa Kamishna, lakini kibali hicho amekitoa kupitia Waheshimiwa Wabunge ambao wameamua wao wenyewe kwamba naweza nikawawakilisha. Sasa nawaahidi kwamba nitawapa ushirikiano mzuri na utumishi uliotukuka na nikuhakikishie kwamba ile dhana kwamba Mheshimiwa Kangi Lugola ana msimamo mkali ni kweli, haiwezekani Wabunge hapa wakakaa wiki mbili hawana chochote, halafu Kangi Lugola akakaa kimya na ni Kamishna.

Kwa hiyo, nawahakikishia kwamba matatizo haya kwa kweli nitatoa ushirikiano kwa Wajumbe wenzangu Makamishina pamoja na wewe Spika tutakupa ushirikiano ili tutatue matatizo ya Wabunge na wafanyakazi wa Bunge hili.

Ahsanteni sana na Mungu awabariki kwa kuniamini kuwa Kamishina wa Tume. Pia niseme kwamba Wakala wangu ambaye nilimwamini, ni wachache sana ambao wewe unakubali wakakutazamie kura, namshukuru Filikunjombe kwa kuwa Wakala ambaye hayumbi na wala hawezi akayumbishwa. Nakushukuru sana Deo Filikunjombe. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Hatujaambiwa kama walipigana huko, acha ushujaa usiokuwa na *tija*. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema niwashukuru sana kwa kazi nzuri tuliofanya mpaka leo ya mambo yetu ya kawaida, kesho ni siku kuu, ni siku kubwa sana. Mabalazi watakuwepo hapa na wageni wengine waalikwa watakuwepo hapa, wengi tu, wamealikwa kwa kadi. Kwa hiyo, inawezekana kesho wageni wa jumla jumla tutaweka na nafasi nyingine katika maeneo mengine kusudi waweze kusikiliza bajeti ya Serikali.

Kwa hiyo, nawatakieni siku njema.

*(Saa 5.30 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 12 Juni, 2014, Saa Tatu Asubuhi)*

***Nakala ya Mtandao (Online Document)***